# Nipashe

Jumatano Septemba 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581796

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**Majaliwa** ataja mikakati mitano kukomesha uharibifu wa mazingira UKURASA WA 3

**Wanakijiji** watiwa mbaroni ugomvi wa wakulima na wafugaji Kilosa UKURASA WA 5

**Darasa** la VII kuanza leo siku mbili za mitihani mipya 'migumu' UKURASA WA 8


LINAVYOAKISI UTAYARI WA CHINA KUIPA AFRIKA VIWANGO VINGINE

siasa

'China ilivyo mbeleko sahihi kuibeba Afrika'

Kujua ufumbuzi wa shida kitaalamu ni mbadala wa wahubiri kiboko ya uchawi

UKURASA 11

DAWA ZA KULEVYA

# Muuzaji wa jumla, tani 1.8 zanaswa



Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lymo

• **Afikishwa** kortini na mama yake wa miaka 70... *Endelea Ukurasa 2*







# Rais Samia, Dk. Malasusa wamlilia Askofu Sendoro

• **Bagonza,** Munga watia neno... *Ukurasa 4*

UKURASA WA 5



## MTAALAMU ATAJA CHANZO ONGEZEKO MATUKIO YA NYUKI KUSHAMBULIA WATU

MKURUGENZI Mtendaji wa Kijiji cha Nyuki Co.Limited amewataka wananchi kuwekeza katika ...

KIFO CHA KIBAO

## Nchi 15 Umoja wa Ulaya zatoa angalizo mauaji yanayoendelea

UKURASA 2

**MICHEZO** **MAYELE: YANGA HII ITAFIKA MBALI CAF** UK.24

**MAONI,** UK.6

# Mabalozi Umoja wa Ulaya watoa tamko matukio ya mauaji

**Na Jenifer Gilla**

MABALOZI wa Umoja wa Ulaya (EU) unaohusisha ubalozi wa Uingereza, Canada, Norway na Uswisi wamekemea matukio ya kutekwa, kuteswa na kuuawa kwa Watanzania yanayoendelea nchini na kuikumbusha serikali kulinda haki za msingi za wananchi.

Aidha, umetoa rai kwa serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhusu matukio hayo ili kuwabaini wahusika.

Tamko hilo limekuja kutokana na kifo cha kutatanisha cha Mjumbe wa Sekretarieti ya Chama cha Demokrasia ya Maendeleo (CHADEMA), Ally Kibao, kilichotokea Jumamosi iliyopita na kuzikwa jana katika kijiji cha Tarigube, Kata ya Togoni, mkoani Tanga.

Inadaiwa kuwa jioni ya Septemba 6, mwaka huu, maeneo ya Kibo Complex Tegeta, jijini Dar es Salaam, akiwa safarini kuelekea nyumbani kwake Sahare, mkoani Tanga na basi la Tashrif, alishushwa na watu waliokuwa na bunduki.

Jumamosi asubuhi mwili wa Ally ulikutwa maeneo ya Ununio, Tegeta mkoani humo ukiwa na majeraha makubwa ikiwamo usoni.

Tamko la pamoja lililotolewa na Umoja huo jana, lilisema wanasikitishwa na vitendo vya ukatili, kupotea kwa watu, na vifo vya wanaharakati wa kisiasa na haki za binadamu na kuishauri serikali kufanya uchunguzi wa haraka kuhusu matukio hayo.

Wameishauri serikali kuhakikisha kuna ulinzi wa vyama vya upinzani, kama alivyoahidi Rais Samia Suluhu Hassan kupitia mpango wake wa R4 ambazo ni maridhiano, mabadiliko, ustahimilivu na kujenga upya, na kulinda haki za msingi za wananchi, ikiwamo uhuru wa kujieleza.

"Jumuiya ya Umoja wa Ulaya inasikitishwa na taarifa za hivi karibuni za vitendo vya ukatili, kupotea kwa watu, na vifo vya wanaharakati wa kisiasa na haki za binadamu. Tunatoa wito wa kufanyika kwa uchunguzi wa haraka kuhusu matukio haya, tunatoa pole kwa familia zote zilizoathiriwa."

Aidha, tamko hilo lilisema matukio hayo yanatishia misingi ya kidemokrasia na haki za wananchi wa nchi hiyo inayoheshimika kimataifa kwa amani na utulivu na kusisitiza wito wa kuendelea kudumisha tunu hizo.

Ulitoa wito kwa Rais wa kuanzisha uchunguzi wa haraka ili kubaini wahalifu waliohusika na matendo hayo na kuhakikisha kuwa wanawajibika kwa unyama huo.


NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street
P. O. Box 6100
Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045
Fax: +255 22 2112045
info@transmark-tz.com
www.transmark-tz.com

Dev Recoveries Ltd

**DEV RECOVERIES LIMITED**

**NOTISI YA MAUZO KWA NJIA YA ZABUNI**

Kampuni ya **DEV RECOVERIES LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED**, tunatoa notisi ya siku kumi nan ne (14) kulipa deni kwa hiari muda huo ukiisha bila kulipa deni hilo dhamana itauzwa kwa njia ya **ZABUNI,** siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini na zabuni itafungwa kama invyoonesha hapo chini:

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA KWA ZABUNI:**

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA ZABUNI KUFUNGWA |
|---|---|---|---|---|
| 01. | BAHASHA MERCHANDISE DEALERS LIMITED | MELCHIADES ALPHONCE RWABUYONGO | Nyumba eneo la Tegeta, , Kitalu namba 668, Dar es Salaam | 30/09/2024 saa 05:00 (Tano) asubuhi |

**MASHARTI YA ZABUNI KAMA INAVYOONYESHA HAPO CHINI.**

1. Mzabuni yoyote anakaribishwa kuleta zabuni kwa ajili ya kununua kwenya bahasha itakayoonyesha ofa yake na anuani ya mzabuni na iletwe kwenye anuani inayoonyesha hapo chini kabla ya saa tano (05:00) asubuhi tarehe 30/09/20234 kwenye ofisi inayoelelzewa hapo chini. Wazabuni mnakaribishwa uwepo wenu wakati wa kufunga zabuni kama utakuwa na nafasi. Zabuni itafunguliwa saa tano na nusu asubuhi siku hiyo hiyo ya tarehe 30/09/2024.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa atalipakilichobaki mnunuzi ndani ya siku 14 au atakubaliana na benki
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 03:00 asubuhi na kuendelea.
5. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
6. Kwa mawasiliano zaidi piga simu No: 0712390460/0712 073 680/0788438640

**MKURUGENZI KUU**
**DEV RECOVERIES LIMITED**
**NIC LIFE HOUSE, 4TH FLOOR, WING C,**
**SOKOINE DRIVE/OHIO STREET**




Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga, Gilbert Kalima akiweka mchanga kwenye kaburi la Saumu Ngome (19) mkazi wa Kijiji cha Perani, Kata ya Mwakijembe aliyeuawa kikatili na mume wake, Sarah Nzuga kwa kutenganishwa kichwa na kiwiliwili, wakati wa maziko yake kijijini hapo juzi. Kulia ni Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, ACP Almachius Mchunguzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Muuzaji wa jumla dawa za kulevya anaswa

**Zanura Mollel na Grace Gurisha**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imetangaza kumkamata inayemtaja kuwa mfanyabiashara wa jumla wa dawa za kulevya nchini.

Mtuhumiwa huyo, Richard Mwanri (47), mkazi wa Mbezi Makonde, wilayani Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, anadaiwa ndiye msambazaji mkuu wa dawa hizo nchini.

"Richard ni mhalifu ambaye amekuwa anapokea dawa za kulevya kutoka nchi mbalimbali na kuingiza nchini kwa usafiri wa magari zikiwa zimefichwa kwa kuchanganywa na bidhaa nyingine kisha kusambazwa kwa wauzaji wengine katika maeneo mbalimbali nchini," amesema Kamishna Jenerali Aretas Lyimo.

Ni alipozungumza na vyombo vya habari jijini jana kuhusu operesheni iliyofanyika kuanzia mwezi uliopita hadi Septemba 2 mwaka huu mkoani Dar es Salaam.

Alisema kuwa katika operesheni hiyo, walikamata kilogramu 1,815 za bangi iliyosindikwa, maarufu skanka.

Pia walikamata watuhumiwa watano wanaohusishwa na dawa hizo, wakiwamo Mwanri na Felista Mwanri (70) ambaye ni mmiliki wa nyumba ambayo inadaiwa dawa hizo zilikutwa.

Watuhumiwa wengine ni Athumani Mohamed (58), mkazi wa Mkoa wa Tanga; Omary Mohamed (32), dereva bajaji na mkazi wa Buza, wilayani Temeke, Dar es Salaam; na Juma Chapa (36), mkazi wa Kiwalani, Dar es Salaam.

Kamishna Jenerali Lyimo alisema kuwa dawa hizo zilikamatwa katika maeneo mbalimbali mkoani hapa, yakiwamo Luguruni, Mbezi na Magomeni.

Kwa mujibu wa DCEA, skanka ni miongoni mwa dawa za kulevya inayotajwa kuwa na kiwango kikubwa cha kemikali zenye sumu aina ya Tetrahydrocannabinol (THC) na huleta athari kwenye mfumo wa fahamu.

"(Skanka) pia huleta matatizo ya akili pamoja na kusababisha magonjwa yasiyoambukiza kama vile maradhi ya moyo, figo na ini. Matumizi ya skanka kwa wajawazito yanaweza kuleta madhara kwa mtoto aliyeko tumboni, ikiwamo kuathiri mfumo wa ubongo na kuzaliwa na uzito mdogo," alisema Kamishna Jenerali Lyimo.

Kamishna Jenerali Lyimo pia alisema kuwa katika operesheni hiyo, walikamata gari aina ya Mitsubishi Pajero lenye namba za usajili T 551 CAB na bajaji yenye namba za usajili MC 844 CZV.

Alirejea taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani iliyotolewa Vienna, Australia mwaka huu, ikionesha kuwa maeneo yaliyohalalisha matumizi ya bangi, yanashuhudiwa kuwa na uzalishaji bidhaa zenye bangi zenye kiwango kikubwa cha kemikali THC.

Kamishna Jenerali Lyimo alisema taarifa hiyo pia imeonesha kuwa nchi zilizohalilisha matumizi ya bangi, zimekuwa na ongezeko la watu wanaohitaji tiba kutokana na matumizi ya bangi sambamba na ongezeka la watu wenye matatizo ya akili na waliojaribu kujiua.

"Mamlaka ipo katika mchakato wa kuvunja mtandao mkubwa wa dawa za kulevya nchini, dawa hizi zinatishia maisha ya watu.

"Pia niombe wamiliki wa nyumba muwe makini na aina ya mzigo mnayopokea katika nyumba zenu," alihadharisha Kamishna Jenerali Lyimo.

**MAHAKAMANI**

Muda mfupi baada ya DCEA kutoa taarifa hiyo, bibi wa miaka 70, Felista Mwanri na mwanawe huyo, Richard (47) na watu wengine watatu walipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa mashtaka ya kusafirisha zaidi ya tani moja ya bangi.

Mshtakiwa Richard alidai mahakamani kuwa mama yake huyo hahusiki, hivyo aachiwe huru; hali ya bibi huyo kwa mwonekano haikuwa nzuri, akisaidiwa kutembea.

Washtakiwa wengine ni Mohamed, maarufu Makame (58) Chapa (36) na Omary (32), waliotajwa awali na DCEA.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Eric Davis alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Godfrey Mhini kuwa washtakiwa hao wanatuhumiwa kwa shtaka moja la kusafirisha dawa za kulevya kinyume cha sheria.

Alidai kuwa washtakiwa wanatuhumiwa kuwa Agosti 28 mwaka huu, wakiwa eneo la Tairo Luguruni, barabara ya Kwembe, ndani ya Wilaya ya Ubungo walikutwa wanasafirisha dawa za kulevya aina ya bangi kilogramu 1,815.

Kuhusu hatua ya upelelezi ilipofikia, Wakili Davis alidai kuwa haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa shauri hilo.

Kuhusu ombi la kuachiwa huru kwa mshtakiwa wa pili, Hakimu Mhini alimweleza mshtakiwa Richard kwamba mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu Mhini aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 24 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

## HABARI KITAIFA

# Majaliwa ataja mikakati mitano kukomesha uharibifu mazingira

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameelekeza mikakati mitano izingatiwe katika kukomesha uharibifu wa mazingira nchini.

Moja ya mikakati hiyo ni maadhimisho ya kitaifa kuratibiwa kwa tija kwa kuwapa elimu watanzania wajue umuhimu wa kutunza mazingira.

Akifunga jana mkutano maalum wa viongozi na wadau kuhusu hali ya mazingira nchini, Majaliwa alisema ni lazima kutumia gharama yoyote kuhifadhi na kutunza mazingira na kusisitiza matumizi ya sheria kusaidia katika kukinga uharibifu wa mazingira uliopo.

"Katika kuratibu matukio makubwa ya kitaifa ikiwamo na maadhimisho ya kitaifa, kuna umuhimu wa kuwa pamoja na maonesho. Wizara sasa itafute namna nzuri ya kukutanisha wadau wa mazingira, itengeneze maonesho yatakayoleta Watanzania wengi kuja kujifunza kwa wiki nzima au mbili ili wajue umuhimu wa kutunza mazingira," alisema.

Majaliwa alisema ni muhimu kwa kila mdau kwa sasa kufuatilia mwenendo wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini.

"Tuanze kwenye eneo lako hali ikoje? Hapa Mkuu wa Mkoa (wa Dodoma, Rosemary Senyamule) ametueleza zamani ulikuwa ukikuta nyumba imepandwa bustani inapendeza unasema hapa ni kwa mzungu. Tumebadilika Watanzania na tubadilike. Watanzania tunataka nyumba kama hiyo yenye mazingira mazuri iwe yako wewe," alisema.

Aliwataka watoe taarifa pindi wanapobaini kuna uharibifu mkubwa wa mazingira kwenye mamlaka za eneo lake.

Alibainisha mkakati mwingine kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wadau ili kulinda mazingira hasa wanapokutana na watanzania wasiokuwa na mapenzi mema wanaoharibu mazingira.

Kuhusu utoaji elimu, Majaliwa alitaka suala hilo liimarishwe na mamlaka husika za masuala ya uhifadhi wa mazingira zijikite kutoa elimu.

"Wadau wa mazingira pangeni ni namna itatumika kufikisha elimu kwa watanzania huko vijijini ili kila mmoja kwenye eneo lake abebe dhamana na mzigo wa kuhifadhi mazingira nchini," alisema.

Waziri Mkuu alisema suala la usafi wa mazingira linapaswa kuzingatiwa na Halmashauri zote nchini kwa kuweka mpango wa wazi ndani ya Baraza la Madiwani ili madiwani wasimamie usafi kwenye maeneo yao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Ashatu Kijaji, alisema hali ya mazingira si nzuri na katika mkutano huo mada nane zimewasilishwa na kutoka na maazimio mbalimbali.

**MAAZIMIO**

Akisoma maazimio ya mkutano huo kwenye makundi tisa, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu na Mbunge wa Kuteuliwa, Dk. Bashiru Ally, alisema wameazimia yafanyike mapitio ya sheria ili kuhuisha sheria zinazokinzana katika uhifadhi wa mazingira ikiwamo sheria ya misitu inayotambua mkaa kama chanzo cha mapato.

"Kuboresha mbinu za kukuza uelewa kwa wizara za kisekta, taasisi za umma na binafsi kuhusu sheria ya usimamizi wa mazingira na kuimarisha utekelezaji wa matakwa ya sheria hii ikiwamo kanuni za mchafuzi kulipa,"alisema.

Pia alisema kufanyika marekebisho ya sheria ili kujumuisha masuala ya biashara ya kaboni na kulifanya Baraza la Taifa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuwa Mamlaka kamili.

Alisema suala la mazingira lipewe kipaumbele cha kwanza kwenye bajeti, Ofisi ya Makamu wa Rais na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziongezewe bajeti na kuwe na ajenda ya kudumu kwenye vikao ngazi za vijiji na Kata.

"Somo la mazingira lihusishe upandaji na utunzaji wa miti, uteuzi wa mfanyakazi bora ujumuishie kigezo cha mchango wake katika hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuanzisha mamlaka za usimamizi wa taka ngumu katika halmashauri," alisema.

Pia alisema uimarishwe udhibiti wa utupaji taka ngumu kwenye vyombo vya usafiri na uchimbaji dawa ili kutunza mazingira.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (katikati), akiangalia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), alipotembelea ofisi za Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa na (katikati) ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala huo, Prof. Neema Mori. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kesi ya Kabendera yatupwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masjala Ndogo Dar es Salalam imetupilia mbali shauri la madai lililofunguliwa na mwanahabari Erick Kabendera dhidi ya kampuni ya mawasiliano Vodacom Tanzania kwa sababu lilifunguliwa nje ya muda.

Kabendera aliomba Mahakama Kuu iamuru kampuni hiyo imlipe Sh. bilioni 28 kwa madai ilifanikisha kutekwa kwake.

Uamuizi huo ulisomwa jana na Naibu Msajili Livin Lyakinana kwa niaba ya Jaji Mfawidhi Salma Maghimbi aliyekuwa anasikiliza kesi hiyo.

Mahakama imetupilia mbali kesi hiyo baada ya kukubaliana na hoja ya pingamizi lililowekwa na Vodacom kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo kwa kuwa imefunguliwa nje ya muda.

Jaji Maghimbi alikubaliana na hoja hiyo akisema kuwa kesi za aina hiyo zinapaswa kufunguliwa ndani ya miaka mitatu tangu kutokea kwa kitendo kinacholalamikiwa, lakini kesi hiyo imefunguliwa baada ya muda huo kuisha.

Alisema mahakama inakubaliana na pingamizi la mdaiwa na kwamba kwa sababu hiyo shauri hilo linafutwa.

Julai 9 mwaka huu, akimwakilisha Kabendera, Wakili Peter Madeleka alidai walalamikiwa Vodacom kupitia Wakili wao Gasper Nyika, waliwasilisha majibu ya madai dhidi yao pamoja na pingamizi wakiomba shauri litupwe.

Jaji Maghimbi aliamuru upande wa wajibu maombi kuwasilisha hoja za pingamizi na ziliwasilishwa Julai 23 mwaka huu.

Mwombaji alijibu pingamizi hilo Agosti 6 na mahakama ikapanga kutoa uamuzi kama shauri hilo liko mahakamani kihalali au la.

Vodacom kupitia Wakili Nyika, walipinga shauri hilo kusikilizwa kwa madai kesi ilifunguliwa nje ya muda wa kisheria, hivyo wakaomba itupwe.

Katika kesi ya msingi, Kabendera alikuwa anaomba mahakama iamuru kampuni hiyo imlipe fidia ya dola za Marekani 10 milioni (sawa na Sh. bilioni 28, akiituhumu kuwa ndio iliyofanikisha kukamatwa kwake na askari polisi, tukio analoliita la kutekwa na kisha kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi mwaka 2019.

Kabendera alidai kuwa kutokana na matukio hayo, amepata madhara ya kiuchumi na yasiyo ya kiuchumi, ya kijamii, maumivu ya kiakili na kimaono, hasara ya kutokufurahia maisha, hasara ya maendeleo binafsi na hadhi yake katika jamii na kutokuaminiwa kitaaluma.

Kwa mujibu wa hati ya madai, Kabendera anadai kuwa Julai 27, 2019, saa tisa alasiri alipowasha simu yake ambayo alikuwa ameizima tangu siku iliyotangulia, ndipo alipobaimi kuwa haikuwa na mtandao.

Mwakilishi wa huduma kwa wateja wa Vodacom alimweleza kuwa namba yake ya simu ya Vodacom (+255767456796) ilikuwa na changamoto za kiufundi ambayo ilimhitaji kutoa taarifa katika kituo cha huduma kwa wateja cha karibu kilichoko Tegeta.

Kabendera alimtaka mwakilishi huyo kuelezea tatizo ni nini kabla ya kwenda huko kituoni, lakini mwakilishi huyo alikataa, akidai kuwa ni suala nyeti ambalo linamtaka aende binafsi kituoni huko.

Badala yake walimshauri atembelee ofisi zao zilizoko Mliman City asubuhi. Hata hivyo, saa tisa alasiri siku hiyohiyo ya Julai 29, 2019, ghafla simu yake ilianza kufanya kazi, kisha alipopigiwa simu na mwakilishi wa Vodacom ambaye alimtaka (Kabendera) amwelezee tatizo lake na baada ya Kabendera kumwelezea kwa takribani dakika tatu, alikata simu akiahidi kumpigia baadaye kidogo.

Baada ya dakika tatu, Kabendera alipokea simu iliyopigwa kutoka huduma kwa wateja Vodacom ambayo aliipokea akabaini kuwa ilikuwa ni sauti ya mwanamume, ambaye alimtaka aeleze mahali alikokuwa na kwamba simu hiyo ilikuwa ikikwaruza kama vile ilikuwa inarekodiwa.

Kabendera anadai kuwa kabla ya simu hiyo kukatwa, alimsikia huyo aliyempigia simu akinong'ona kuwa "yuko nyumbani kwake" na kuongeza kuwa "sogea karibu na nyumba yake".

Kwa mujibu wa hati hiyo, maelezo hayo yalimshtua Kabendera na akakimbia sehemu ya juu ya nyumba yake. Akiwa huko, aliona magari kadhaa ambayo hakuyafahamu karibu ya nyumba yake.

Kisha lilitokea gari lingine aina ya Toyota Alphard lililoegesha mbele ya magari hayo upande wa kulia mwa nyumba yake; wakashuka watu wanne ambao walijitambulisha kuwa maofisa wa polisi lakini walikataa kutoa utambulisho. Walimfunga pingu na kumshikilia kizuizini kwa siku mbili.

Wakati wa mahojiano, maofisa wa polisi walifika katika chumba cha mahojiano wakiwa na karatasi zilizochapishwa kutoka katika kompyuta (printout) za akaunti za fedha ya simu na namba za simu alizokuwa amezipigia kwa mwaka mzima.

Hivyo, walimhoji lengo la kila muamala aliofanya kwa mwaka mzima, pia uhusiano wake na watu aliokuwa amewasiliana nao miaka kadhaa.

Analalamika kuwa polisi na serikali walitoa taarifa kadhaa zenye mgogoro kwa umma kuhusiana na 'kutekwa' kwake na kwamba walimtuhumu kwa kutokuwa raia na kumkashfu Rais (wa wakati huo) Dk. John Magufuli.

Anadai alishtakiwa mahakamani kwa makosa ya utakatishaji fedha, uhujumu uchumi na ukwepaji kodi na matokeo yake walimweka chini ya ulinzi mkali katika mahabusu ya Gereza la Segerea, jijini Dar es Salaam.

Inaelezwa zaidi katika hati hiyo kuwa wakati akiwa mahabusu, mama yake, Verdiana Mujwahuzi alifariki dunia na hakuruhusiwa kuhudhuria mazishi yake na kwamba hata yeye mwenyewe alikuwa na tatizo la kiafya.

Anadai katika hati hiyo kutokana na hali hiyo aliamua kukiri makosa na kulipa fidia ya Sh. milioni 273 ili atoke mahabusu na kwamba baada ya kuachiliwa marafiki na familia yake walimweleza kuwa walipigiwa simu na polisi wakiwaonya kutomtembelea mahabusu, vinginevyo wangejiweka hatarini.

# Malasusa, Samia wamlilia Askofu Sendoro

**Na Godfrey Mushi,**

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa, na Rais Samia Suluhu Hassan, wamemlilia aliyekuwa Askofu wa Dayosisi ya Mwanga ya kanisa hilo, Dk. Chediel Sendoro, aliyepoteza maisha juzi kwa ajali ya gari.

Dk. Sendoro ni mtoto wa Askofu wa Kwanza wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Elinaza Sendoro.

Sambamba na viongozi hao, mwingine aliyetoa ujumbe wa huzuni ni rafiki yake wa karibu, Askofu Dk. Benson Bagonza wa KKKT Dayosisi ya Karagwe mkoani Kagera aliyesema "mwanga wa Mwanga umezimika."

Katika salamu zake za rambirambi kwa wakristo wa KKKT na umma, Askofu Dk. Malasusa amewaomba kuendelea kuiombea familia, KKKT Dayosisi ya Mwanga, wana KKKT na wote walioguswa na msiba huo.

"Lakini ndugu, hatutaki msijue habari za waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini (1 Wathesalonike 4:13)."

Kutokana na kifo hicho, Rais Samia ametuma salamu za pole kwa Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Malasusa, maaskofu wote, waumini, familia, ndugu, jamaa na marafiki.

Kupitia Mtandao wa X, Rais Samia aliandika: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Baba Askofu Chediel Elinaza Sendoro, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mwanga. Natoa pole kwa Mkuu wa KKKT Baba Askofu Dk. Alex Gehaz Malasusa, maaskofu wote, waumini, familia, ndugu, jamaa na marafiki.

"Nawaombea faraja kwa neno kutoka katika Biblia Takatifu Kitabu cha Waebrania 13:14 kwamba 'Maana hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao.' Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi."

**BAGONZA, MUNGA WAOMBOLEZA**

Askofu Dk. Bagonza katika ukurasa wake wa Facebook aliandika: Mwanga wa MWANGA Umezimika. Askofu Chedy Sendoro umeniacha porini. Ulikuwa Mwanga wa Wana Dayosisi ya Mwanga. Ulikuwa chachu ya wana Utatu - Karagwe, Mwanga na Pare. Kuondoka kwako kunafifisha mwanga wa wana Utatu.

"Wewe ni mwana KKKT. Mzaliwa wa kwanza wa Dayosisi namba 25 ya Mwanga. Kiungo halisi katika nyumba ya Maaskofu. Kipenzi cha kila Askofu. Kumchukia yeye ni kujichukia. Umeacha alama kote katika Mwanga, KKKT, CCT, na katika Utatu wetu. Ulikuwa na deko kwa sababu una wazazi, ulipendeka kwa sababu hukuwalazimisha waliokupenda.

"Ulikuwa na nafasi ya pekee kwangu: Uliweza kuniambia nisiyoweza kuambiwa na wengine. Uliponyamaza tulihisi unaharibu kitu. Ulipofurahi tulijua kuna jambo laja. Ulijaliwa kusema ukweli bila kuudhi kama wengine tulivyo. Ulipendwa na wanaokujua



Marehemu Askosfu Chediel Sendoro

na wasiokujua. Ama kweli anajua kuvuna kilicho bora na kutubaliza magarasha. Wapo ambao wakiondoka pengo lao linazibika. Lako tutaliziba lakini kivuli chako kitatutesa."

Askofu Mstaafu wa KKKT, Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Dk. Stephen Munga, alisema: "Leo nimempoteza ndugu na rafiki wa kipekee. Tunatoa pole kwa mke wake na watoto wake Erica na Eric. Tunaendelea kuwaombea faraja; na pia tukimuombea mtoto wao Eric ambaye alipata majeraha katika ajali hiyo iliyosababisha mauti kwa baba yake."

**AJALI ILIVYOKUWA**

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Simon Maigwa, Askofu Sendoro, alifariki dunia usiku wa Septemba 9, mwaka huu, saa 1:30 usiku, baada ya gari alilokuwa akiliendesha aina ya Toyota Prado, kugongana uso kwa uso na lori aina ya Scania katika eneo la Kisangiro, wilayani Mwanga.

Kamanda Maigwa, alisema kabla ya kupoteza maisha, Askofu Sendoro na mwanawe ambaye anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, alikuwa akitokea katika mji mdogo wa Himo, wilaya ya Moshi kwenda Mwanga.

Alisema gari lake lilikuwa likiyapita magari mengine mawili na kisha kugongana uso kwa uso aina ya Scania lililokuwa likitokea Tanga kwenda mkoani Arusha.

**MAISHA YAKE**

Askofu Sendoro, ambaye hadi anafariki dunia alikuwa mhitimu wa shahada ya uzamivu (PhD) na shahada ya juu ya uhasibu (CPA), alizaliwa Mei 1, 1970 akiwa mtoto wa nne wa Askofu Dk. Elinaza Sendoro.

Mwaka 1991, baada ya kuhitimu kidato cha sita, alijiunga na Chuo cha Taifa cha Uhasibu (TIA), wakati huo kikiitwa Shule ya Uhasibu Dar es Salaam (DSA), kusomea stashahada ya juu ya uhasibu (ADA) na kuhitimu mwaka 1995.

Mwaka 1997 alihitimu CPA kutoka Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA) na kuajiriwa kama Mhasibu Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT).

Lakini mwaka 2000, alitumwa na kanisa kwenda Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, kusomea Shahada ya Theolojia kwa miaka mitano na kuhitimu 2006. Alibarikiwa kuwa Mchungaji wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP) kisha akarudi Makumira kwa shahada ya umahiri katika Theolojia na kuhitimu mwaka 2008.

Alirudi DMP na kupewa majukumu ya kuongoza idara ya Misoni na Uinjilisti. Baadaye aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Dayosisi nafasi aliyoitumikia hadi mwaka 2012, alipokwenda masomoni Chuo Kikuu cha Abo Academy, Finland kusomea Shahada ya Uzamivu ya Theolojia. Mwaka 2015 alichaguliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Fungamano la Kimataifa la Injili (UEM) Kanda ya Afrika yenye makanisa 39. Mwaka 2016 Dayosisi ya Mwanga ilizaliwa kutoka Dayosisi ya Pare na Mkutano Mkuu ulimchagua kuwa Askofu. Aliwekwa wakfu na Novemba 6, 2016 na hatimaye kuingizwa kazini na aliyekuwa Mkuu wa KKKT wakati huo, Askofu Dk. Fredrick Shoo.

Askofu Dk. Sendoro, ameacha mjane na watoto wawili, (Erica na Eric).


IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA

AT DAR ES SALAAM

CIVIL CASE NO. 16400 OF 2024

TATA AFRICAN HOLDINGS .................................................. APPELLANT

*versus*

SAID ALBUSADY LIMITED............................................RESPONDENT

TO:

SAID ALBUSADY LIMITED

DAR ES SALAAM

SUMMONS FOR PUBLICATION

**WHEREAS**, the Applicant has instituted a suit against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by a pleader duly instructed and able to answer all material question relating to the suit or who shall be accompanied by some person able to answer all such question on the 03rd day of October, 2024 at 9:00 am, before **Hon. A. J. KIREKIANO, JUDGE** for Mention.

**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on the day before mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of court this 2nd day of September, 2024.

THE HIGH COURT OF TANZANIA

DEPUTY REGISTRAR

DAR ES SALAAM ZONE


# CCM yalaani kada kuchomewa mali

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimelaani kitendo cha kuchoma moto mali za mwanachama wake mpya kutoka ACT-Wazalendo, Salum Mohamed Juma, katika shehia ya Wingwi Mapofu, Wilaya ya Micheweni, Pemba.

Kutokana na kitendo hicho, kimelitaka Jeshi la Polisi kuchukua hatua za kisheria kwa watu wote waliohusika na vitendo.

Pia kimesema baadhi ya wanachama wapya wa CCM wameanza kutishwa na kufanyiwa vitendo vya hujuma na wengine kujeruhiwa na kuharibiwa mali zao hali inayotakiwa kudhibitiwa na vyombo vya ulinzi na usalama.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa, alisema hayo jana baada ya kuweka jiwe la msingi katika Maskani ya CCM Mjini Kiuyu, Jimbo la Kojani, katika mwendelezo wa ziara ya kikazi ya kuimarisha chama ya Wajumbe wa Sekretarieti ya Kamati Maalum ya NEC Zanzibar katika wilaya ya Wete Kichama.

Watu wasiojulikana, juzi walivamia makazi ya Salum na kuingia nyumbani kwake kisha kuchoma moto godoro, vitambulisho, nguo na bendera ya CCM hatimaye kukimbia baada ya wananchi kujitokeza kuzima moto uliokuwa umeanza kuchoma makazi yake.

Dk. Dimwa ametoa pole kwa mwanachama huyo na wengine wanaopata vitisho na kauli za ubaguzi ambapo amewahakikishia kuwa watakuwa na usalama wa mali na maisha yao ya kila siku.

Kutokana na tukio hilo, alisema CCM inatarajia vyombo vya ulinzi na usalama vitachukua hatua za haraka kwa kuhakikisha watu wote waliohusika bila kujali, cheo, chama cha kisiasa na umaarufu wanafikishwa katika vyombo vya sheria.

Amesema Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliundwa kwa dhamira ya kumaliza siasa za chuki na visasi ili kuweka nchi katika hali ya amani na utulivu na kuhakikisha nchi inapiga hatua kimaendeleo na wananchi wanaishi kwa amani.

# Zaidi viongozi 300 kujadili mabadiliko ya akili bandia sekta mbalimbali

**Na Mwandishi Wetu**

MKUTANO wa Kimataifa wa Akili Bandia (Global AI 2024), unaoandaliwa na Mamlaka ya Saudia ya Akili Bandia (SDAIA), umeanza jana mjini Riyadh, Saud Arabia, kukuza ushirikiano wa kimataifa na kuangalia uwezekano wa kuleta mabadiliko ya Akili Bandia katika sekta mbalimbali.

Kwa mujibu wa Balozi wa Saudi Arabia nchini, Yahya Bin Ahmed Okeish, mkutano huo ambao unaenda sambamba na Dira ya Saudi Arabia ya 2030 unatarajia kumalizika Septemba 12 na kuwaleta pamoja viongozi zaidi ya 300 wa akili bandia.

"Mijadala ya wazungumzaji zaidi ya 300 wakiwamo wavumbuzi, wasomi, watendaji, wadhibiti na watoa maamuzi kutoka nchi 100 itazingatia Kaulimbiu ya mkutano huo isemayo; "Sasa, ifuatayo, Kamwe".

Vikao vitajadili athari za mabadiliko ya teknolojia kwa watu na jamii, faida halisi inayopata dunia kutokana na Akili Bandia, mwelekeo wa teknolojia wa siku zijazo na umuhimu wa kuzingatia maadili ili kuhakikisha kuwa uwajibikaji wa maendeleo katika sekta zote.

Mkutano huo utajumuisha safu ya wazungumzaji wa kimataifa ikiwa ni pamoja na Cristiano Amon, ambaye ni Rais na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Qualcomm Incorporated, Nick Studer, Rais na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Oliver Wyman Group, Dk. Marc Raibert ambaye ni Mwenyekiti wa Kampuni ya Boston Dynamics, Marcelo Claure ambaye ni Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Claure Group na Julie Sweet ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Accenture.

Wengine ni Amandeep Gill, Mjumbe wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu masuala ya Teknolojia, Kathleen Kennedy ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha MIT cha akili ya pamoja, Alex Smol ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Boson AI, Andrew Feldman, Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Cerebras Systems, Dk. Chris Miller, Mkurugenzi wa kampuni ya Greenmantle na Caroline Yap, Mkurugenzi Mkuu wa Kimataifa kutoka kampuni ya Google Cloud.

Pia, wamo Stefan Schnorr ambaye ni Waziri wa Nchi anayeshughulikia masuala Dijiti na Uchukuzi ya Shirikisho la Ujerumani, Charles-Edouard Bouée, Mwanzilishi Mwenza na Mshirika Msimamizi wa kampuni ya Adagia, Jonathan Ross ambaye ni mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Groqna, Dk. Deepak Chopra ambaye ni mwanzilishi wa taasisi ya Chopra.

Wakati huohuo, Msemaji Mkuu wa Mamlaka ya Saudi Arabia ya Akili Bandia(SDAIA), Mhandisi Majed Al-Shehri, amesema mkutano huo utakuwa ni tukio la kihistoria katika kuunda mustakabali wa Akili Bandia, na kwamba Kaulimbiu ya "Sasa, Ijayo, Kamwe" ni muhimu sana kwa kuwa inawapa changamoto ya kuangalia athari za haraka, uvumbuzi wa siku zijazo, na majukumu ya kimaadili yanayokuja na maendeleo ya haraka ya teknolojia ya Akili Bandia.

"Hii ni teknolojia ambayo inatia matumaini sana, lakini tunapovumbua, pia hatuwezi kumudu kuikosea. Ni muhimu kwamba ushirikiano wa Akili Bandia uwe endelevu na kwa ajili ya kuboresha jamii. Ushiriki mkubwa wa viongozi wa kimataifa, hasa kutoka katika tasnia ya ushauri unaonesha jukumu muhimu la Akili Bandia katika mabadiliko ya biashara na uvumbuzi wa kimataifa na kujitolea kwao kwa ushirikiano katika kipindi ambacho tunatafuta namna ya kutatua maswali mengia mbayo teknolojia hii inayaibua," alisema.




Mkuu wa Kitengo cha Mauzo Pumagas kutoka kampuni ya Puma Energy Tanzania, Jeffrey Nasser (kulia) na Meneja Masoko, Lilian Kanora (wapili kulia) wakimkabidhi mtungi wa gesi Faith Amri (wapili kushoto), wakati wa kampeni ya kutokomeza matumizi ya mkaa kama nishati ya kupikia iliyofanyika Mbagala, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtaalamu ataja chanzo ongezeko matukio ya nyuki kushambulia watu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKURUGENZI Mtendaji wa Kijiji cha Nyuki Co.Limited amewataka wananchi kuwekeza katika sekta ya ufugaji nyuki ili kukabiliana na ongezeko la nyuki ambao wameanza kuingia katika makazi ya watu, nyumba za ibada na kuwashambulia watu, wakiwajeruhi na wakati mwingine kusababisha vifo.

Philemon Kiemi alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kufuatia tulio la hivi karibuni la watu kushambuliwa na nyuki eneo la Mbweni, Dar es Salaam na kuwajeruhi. Alisema hivi sasa kuna ongezeko kubwa la makundi ya nyuki ambao wanazagaa kwenye makazi ya watu, misikiti, makakisa, shule, minara ya simu na maeneo mengine na hali hii inatokana na kwamba wamekosa sehemu ya kwenda kwa sababu hakuna mazingira maalum yaliyoandaliwa kuwatunza.

"Matukio ya watu kushambuliwa na nyuki hivi karibuni yameripotiwa kutokea katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Singida, Kagera na Shinyanga, hali hii inajitokeza kwa sababu makundi ya nyuki ambayo yalitakiwa kufugwa na binadamu, lakini binadamu hawa hawafanyi jitihada za kuwatengenezea nyuki makazi, ikiwamo mizinga," alisema.

Kiemi alisema njia pekee ya kuwafanya nyuki kurudi msituni ni kutengeneza mizinga ya kisasa itakayowavutia kuingia humo na kutenga maeneo maalum ya kuwafuga ambapo jitihada hizo zisipochukuliwa, matukio ya watu kushambuliwa na makundi ya nyuki yataendelea.

Alisema katika Mkoa wa Singida pekee, kunakadiriwa kuwa na makundi ya nyuki 900,000 lakini makundi ambayo yamo katika mizinga ni 240,000, hivyo makundi yaliyobaki, zaidi 600,000 yanaishi katika majabali, miti, makazi ya watu, shuleni, misikitini na kanisani.

Kiemi alisema katika kipindi cha takribani miaka 10, zaidi ya watu 10 wamefariki dunia mkoani Singida kutokana na kushambuliwa na nyuki.

"Safari wanazofanya nyuki kwenda kutafuta maji na safari zinafanana na safari wanazotumia kwenda kutafuta malisho, hivyo sisi watalaamu tumeamua kutengeneza mizinga ambayo ina sehemu ya kuweka maji ili kuwapunguzia safari nyuki kwenda kutafuta maji," alisema.

Mtaalamu huyo alisema hatua hiyo itamwezesha mkulima kuvuna asali zaidi ya mara moja.

Kiemi alisema njia nyingine ya kukabiliana na matukio ya kushambuliwa na nyuki ni wananchi kupewa elimu, mtu anaposhambuliwa na nyuki anatakiwa kusaidiwa vipi ili asipate madhara makubwa zaidi.

"Mtu akishambuliwa na nyuki, hatua ya kwanza ni kumwondolea miba ya nyuki ili sumu isiingie zaidi mwilini mwake na hatua ya pili ni kumpa maji na kumpeleka kwenye chumba chenye giza.

"Watu wasichukulie nyuki kuishi kwenye dari ni baraka, hapana! Ni sababu wamekosa sehemu maalum pa kwenda," alisema.

Kiemi alisema kuwa kutokana na ongezeko hilo la nyuki, wananchi hivi sasa wajenge tabia ya kutembea na vifaa vya kujikinga na nyuki wanapokwenda kazini na kwenye magari, kama tahadhari ya kukabiliana nao wanaposhambuliwa.

Alisema Kijiji cha Nyuki Co. Limited kimejipanga kuwafundisha asilimia 75 ya Watanzania ili waweze kuingia katika sekta ya ufugaji nyuki na pia waweze kulima mazao kama alizeti ambayo hayaathiri nyuki.

Alisema kuwa hivi sasa wananchi wengi wameanza kujitokeza kuingia katika sekta ya kufuga nyuki baada ya kutambua kuwa ufugaji wa nyuki hauna gharama sana, ni kuwa na mzinga tu.

# Wananchi 12 watiwa mbaroni vurugu za wakulima, wafugaji

**Na Idda Mushi,** KILOSA

WANANCHI 12 wakazi wa Kijiji cha Malangali, Kata ya Tindiga, wilayani Kilosa, mkoani Morogoro, wanashikiliwa na vyombo vya ulinzi na usalama huku wengine wanane wakitafutwa baada ya kuibuka vurugu baina ya wafugaji na wakulima kijijini huko.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka alitoa taarifa hiyo jana wakati anazungumza na waandishi wa habari na kuonya kuwa serikali haitaruhusu mtu yeyote kujichukulia sheria mkononi.

Alisema wanatarajia kukutana na viongozi wa wafugaji katika wilaya hiyo wakati wowote na kusisitiza wakulima nao kutafuta uongozi wa kushughulikia changamoto zinazowakabili, zikiwamo za ardhi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Malangali, Seleman Mapala alisema vurugu hizo zilitokea Septemba 8 mwaka huu baada ya wafugaji kudaiwa kuingiza mifugo katika mashamba ya wakulima na wakulima kuamua kukamata mifugo hiyo.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Kata ya Tindiga, Abiuda Karao alisema kuwa ili kudumisha amani na utulivu, wananchi wanatakiwa kuwa wamoja na kuheshimiana kwa kuwa baadhi ya wafugaji wamezaliwa katika eneo hilo.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Naibu Kamishina wa Polisi (DCP) Mihayo Msikhela aliyeonya kuwa jeshi hilo halitamvumilia mtu yeyote atakayevunja sheria.

Naibu Kamishna Mihayo alitaka wananchi kila mmoja kuheshimu sheria za nchi na kuonya kuwa kujichukulia sheria mkononi ni kuvunja sheria na kamwe hawatavumilia.

Kilosa ni miongoni mwa wilaya zinazokabiliwa na migogoro ya wakulima na wafugaji licha ya hatua kadhaa zilizochukuliwa na serikali, ikiwa ni pamoja na kuundwa Timu ya Mawaziri Wanane wa Kisekta mwaka 2019.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Polisi iwajibike ipasavyo katika kukomesha vitendo vya uporaji

**HIVI** karibuni imeripotiwa katika baadhi ya vyombo vya habari kwamba kumekuwa na ongezeko la vitendo vya uporaji wa vitu mbalimbali vikiwamo simu za mkononi ma mikoba kupitia pikipiki ya abiria, maarufu bodaboda.

Uporaji huo umekuwa ukifanywa na madereva wa pikipiki hizo kwa kuvizia watu waliosimama kwenye vituo vya mabasi wakisubiri usafiri wa kwenda sehemu mbalimbali ama nyumbani, kazini au kwenye sherehe.

Wenye bodaboda hao, pia huwafuatilia kwa nyuma watu walioko kwenye mabasi ya abiria maarufu kama daladala na bajaji zinazosafirisha abiria kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Wakati wa kufanya uhalifu huo, madereva hao huwa na watu nyuma ambao huwafanya kama abiria na wanapofika sehemu husika, hupora mikoba au simu na wale wanaojaribu kuzuia kuibiwa huburuzwa na kupata majeraha sehemu mbalimbali za miili.

Kwa ujumla, vitendo hivi vimeshamiri katika maeneo ya miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Watu hao hupita katika barabara kubwa zenye magari mengi ya abiria. Baadhi ya wanaofanya vitendo hivyo, wanapofika kwenye vituo, hujifanya wanatafuta abiria wa kuwaunganisha na wale walioko nyuma kumbe nia yao ni kuangalia wanaotumia simu wakati huo au wenye mikoba ya kompyuta na ile ya kinamama.

Mkoani Dar es Salaam, mathalan, maeneo ambayo yameripotiwa kukithiri kwa vitendo hivyo ni Kinyerezi Mwisho, Mabibo External, Banana, barabara ya Maji Chumvi kutoka External hadi Bosnia, Riverside, Kimara, Mpakani maarufu kama Mwenge Vinyago na barabara ya Morogoro.

Vitendo hivi ni sehemu ya matukio ya uhalifu yanayoendelea katika miji na kurudisha nyuma maisha ya wananchi kama ilivyo kwa vikundi vya Komando Yosso, Tukale Wapi, Kiboko Msheli, Panya Road na Wadudu ambavyo vimekuwa tishio kwa maisha ya wanadamu na mali zao. Kilio hicho kimesikika katika ngazi mbalimbali za jamii vikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo baadhi, kama Jeshi la Polisi, vimekiri kuwapo kwa jambo hilo huku vikiwasisitiza wananchi waliokumbwa na mikasa hiyo watoe taarifa ili hatua ichukuliwe dhidi ya wanaofanya vitendo hivyo.

Si kwamba vitendo hivyo havifahamiki kwenye vyombo vya usalama bali taarifa za wahusika na majina yao yako kwenye vituo mbalimbali vya polisi. Kwa mantiki hiyo, kama ni kuvikomesha ni rahisi lakini kwa sababu baadhi ya askari wasio waaminifu wananufaika navyo, inakuwa nguvu kuvikomesha, hivyo vinaendelea na uporaji na hata kugharimu maisha ya wananchi.


Jambo hilo ni dhahiri kwa sababu miaka kadhaa iliyopita, ofisa mwandamizi mstaafu wa polisi aliporwa simu yake eneo la Fire na alipotoa taarifa ndani ya muda mfupi magari ya polisi yalifika eneo hilo na kuwahadharisha vibaka kuwa simu waliyoipora ni ya mkubwa, hivyo wairudishe na siku hiyo hiyo, saa zisizozidi tatu ilipatikana.

Kutokana na ukweli huo, ni vyema Jeshi la Polisi likachukua hatua stahiki katika kutokomeza uhalifu huo kwa sababu baadhi ya wanaofanya vitendo hivyo wanajulikana na hata pikipiki wanazotumia kufanya uporaji huo zinajulikana. Kwa mantiki hiyo, Jeshi la Polisi kama litadhamiria kupambana na uhalifu wa aina hiyo, matokeo chanya yanaweza kupatikana ndani ya muda mfupi.

Wahenga wanasema penye nia pana njia. Kwa msemo huo, kama kweli Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na watoa taarifa litadhamiria kukomesha vitendo hvyo, ni dhahiri kwamba haitachukua muda wahusika watafichuliwa na kutiwa mbaroni hatimaye kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Sambamba na hilo, wale wanaobainika kuhusika na vitendo hivyo, vyombo wanavyovitumia kufanikisha matukio hayo vitaifishwe ili kuwa fundisho kwa wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Moshi Lusonzo

# Watanzania wanahitaji anachotaka Rais

**TANGU** mjumbe wa Sekretarieti wa CHADEMA Taifa, Ali Kibao, kuuawa kikatili wiki iliyopita Septemba 6, hali ya wasiwasi inazidi kutanda , watu wengi wakipata hofu ya usalama wao hasa wanaharakati na watetezi wa demokrasia.

Kifo hicho cha kushtua kimezidi kuleta utata kuhusu matukio mengi ya utekaji, kuua na kutoweka kwa baadhi ya watu ambao hadi sasa hakuna taarifa kamili kuhusu wapi walipo na kitu gani kimewakabili.

Kitendo cha kutekwa Kibao akiwa ndani ya basi akielekea Tanga tena kwa mtutu wa bunduki na hatimaye mwili wake kukutwa umetupwa eneo la Ununio mkoani Dar es Salaam, ni kuongeza taharuki, hofu, wasiwasi na kuipa Tanzania jina jingine linaloweza kutofautiana na kisiwa cha amani.

Watu wanaweza kuamini kuwa wanaofanya unyama huo wana uhuru mkubwa wa kutenda chochote na lolote , wakati wowote na mahali kokote bila hofu.

Watanzania wengi wana maswali mengi ambayo hayana majibu, wamebaki na tumaini moja pekee nalo ni kutekelezwa maagizo ya Rais Samia Sulu Hassan, ambaye ameamuru kufanyika uchunguzi wa haraka na kina kuhusu tukio hilo.

Ni wazi Rais Samia, amezungumza kutoka moyoni na anahisi maumivu makali kutokana na matukio ya aina hayo kuendelea nchini yanayofanywa na watu waliojipachika jina la wasiojulikana.

Baada ya kauli yake hiyo ambayo aliagiza vyombo vya uchunguzi kumpelekea taarifa ya kina kuhusu tukio hilo, ni wazi majibu yatapatikana na kuwapa auheni wengi wanakata tamaa na kuzidiwa na hofu.

Ukweli mama ameshazungumza na hakuna ambaye anaweza kwenda kinyume na hitaji lake, na ndivyo wengi wanatamani kuona ili kukata kiu yao ya muda mrefu ambayo inazidi kuwatesa wanaharakati na wanasiasa.

Kama ilivyo kwa Rais Samia ambaye naye anatamani kujua nini kipo ndani ya tukio hilo, Watanzania pia wanataka kujibiwa maswali ambayo yanawapa shida kupata majibu ikiwamo watu gani wametekeleza unyama huo? Ni nani yuko nyuma na wanaofanya matukio hayo? Sababu yake ni nini?.

Pia, wanataka kufahamu kama watu hao wasiojulikana wanaweza kutekeleza misheni yao kwa uhuru hata katika maeneo ya umma, ndani ya chombo cha usafiri kilichosheheni abiria.

Kuna wanaonyooshea kidole vyombo vya dola kuwa pengine vinahusika, lakini majibu atakayopelekewa Rais Samia yanaweza kutoa mwanga na kisha kuwaondoa shaka raia ambao kwa sasa wamebaki njia panda.

Ukweli ni kwamba uchunguzi huo ambao umeagizwa kufanywa na vyombo vya dola, utarudusha hali ya kuaminiana ambao kwa sasa umeonekana kutoweka baada ya kushamiri kwa matukio ya watu kutekwa na kuawa kimya.

Kimsingi Watanzania wanamuunga mkono kwa dhati Rais Samia kutaka kupata maelezo ya kina na kuhusu kilichotokea kabla na baada ya kuawa Kibao ambaye familia yake na taifa kwa ujumla bado lilihitaji mchango wake.

Pamoja na wengi kutokubaliana na hali inavyoendelea, lazima tujiweke kando na vitendo vyovyote vya kuingilia mwenendo wa uchunguzi na ikiwezekana wale wenye vielelezo au taarifa zinakazowabaini wahusika kujitokeza kwenda kuwasilisha sehemu husika.

Hakuna njia nyingine nzuri ya kurahisisha mchakato huo, bali ni kushirikiana na timu inayochunguza tukio hilo na kisha majibu yake kuwasilishwa kwa rais.

Ni wazi Rais hajatoa agizo hilo kwa kujifurahisha, bali anaona umefikiwa wakati matukio ya aina hayo kukomeshwa kwa ajili ya maslahi ya nchi na uimara wa demokrasia na amani ya taifa.

Hakuna Mtanzania anayekubali kuona vitendo vya aina hii vikiendelea kuiumiza nchi, hivyo ni lazima vyombo vya dola vinavyohusika kulinda usalama wa watu kuingilia kati ili watu waendelee kuishi kwa amani na kufanya shughuli zao kwa uhuru.

Wakati umefika kwa jeshi la polisi ambalo wengi wanalilalamikia kwa kutofanya kazi ipasavyo katika kukabiliana na vitendo vya utekaji, kubadili mbinu zake kwa kuwatufuta watu hao na kuwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sharia kabla hajatekeleza malengo yao.

Waanzishe madawati huru ambayo wananchi wanaweza kwenda kutoa taarifa bila kuwa na hofu au kuonesha viashiria ambavyo vitabaini kufuatiliwa, kuwaona watu wanaotiliwa shaka.

HABARI KITAIFA

## Mshtakiwa akwamisha kesi mahakamani

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeshindwa kuendelea kusikiliza kesi ya tuhuma ya kujeruhi na kutoa lugha ya matusi, kutokana na mke wa mshtakiwa Bharat Nathwan (57), Sangita Bharat (54) kuwa mgonjwa.

Imedaiwa mahakamani huko kuwa Sangita, kutokana na maradhi, hawezi kumsikiliza shahidi wa upande wa mashtaka.

Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania wenye asili ya India wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana, Dar es Salaam, wanaotuhumiwa kwa mashtaka manne waliyoyatenda Julai 21, 2023 kinyume cha sheria.

Taarifa hiyo ilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Aaron Lyamuya wa mahakama hiyo na Wakili wa washtakiwa hao, Edward Chuwa wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa shahidi wa tano wa upande wa mashtaka.

"Mheshimiwa tupo tayari kuendelea. Isivyo bahati, tumepata habari mteja wangu Sangita ni mgonjwa, anasumbuliwa na presha na nimonia, lakini alitamani kushiriki kwenye kesi, tunaomba akapumzike.

"Tunaomba ahirisho ili mteja aende kupumzika nyumbani na pia tuna vyeti vya ugonjwa," alidai Wakili Chuwa.

Akijibu taarifa hiyo, Wakili wa Serikali Faraja Ngukah, alidai kuwa suala la afya ya mtuhumiwa hawawezi kulipinga na kwa sababu wakili kadai ana vyeti, basi viletwe kama sheria inavyoelekeza.

"Kama anaumwa na wamekubalina na wakili wake haina shida, nimeona hivi vyeti vimeandikwa jina la Sangita na ndiyo mtuhumiwa, siwezi kusoma karatasi hizi nikasema anaumwa nini, tunaomba tarehe nyingine ya kusikilizwa," alidai Wakili Ngukah.

Baada ya Ngukah kudai hayo, Wakili Chuwa alipendekeza Septemba 26, 2024 ndiyo kesi iendelee kusikilizwa, walikubaliana tarehe hiyo na mahakama ikaahirisha.

"Shahidi ninakuonya, ufike mahakamani Septemba 26, 2024 kuja kutoa ushahidi mahakamani hapa, ufike bila kukosa," aliagiza Hakimu Lyamuya.

Iidaiwa kuwa Nathwan anatuhumiwa kuwa Julai 21, 2023, akiwa eneo la Mtaa wa Mrima-Kisutu, jengo la Lohana, ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, kinyume cha sheria alimsababishia madhara Kiran Lalit kwa kuzamisha kichwa chake katika ndoo yenye saruji iliyochanganywa.



Katibu wa Halmashauru Kuu ya CCM Taifa (NEC), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makala (kushoto) na Mbunge wa Kiteto, mkoani Manyara, Edward Ole Lekaita, wakiingia kwenye viwanja vya Kata ya Engusero juzi, kwa ajili kusikiliza kero za wananchi na kukagua uhai wa chama. **PICHA: GIFT THADEY**

# CCM yaonya kamati za siasa kuchagua kwa upendeleo

## -Waliouza ardhi ya wananchi kukatwa

**Na Salome Kitomari,**
SIMANJIRO

KATIBU wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, ameelekeza Kamati ya Siasa za Wilaya za chama hicho, kutotumia vibaya madaraka yao kwa kuchagua wagombea wa Serikali za Mitaa kwa upendeleo.

Akizungumza jana na mabalozi, madiwani, wajumbe wa kamati ya siasa wilaya na mkoa, viongozi wa jumuiya za chama hicho, mkuu wa wilaya, wabunge na viongozi wengine katika Mji wa Orkesumet, wilayani Simanjiro, Makalla alisema ni lazima dhamana hiyo waitumie vizuri.

Alisema iwapo watapitisha mgombea ambaye anaongoza kusababisha kero, baada ya majina kutajwa, wana CCM wataanza minong'ono na kuwa kwenye uelekeo wa kushindwa, ndio maana wanatakiwa wagombea safi.

Alisema kwa chama hicho hivi sasa hakuna ajenda nyingine muhimu zaidi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Makalla alisema ahadi ya kumchukulia fomu ya kugombea urais iliyotolewa na wana Simanjiro itakuwa na nguvu iwapo watampa vitongoji na vijiji vyote kuwa na viongozi wa CCM.

"Wamasai ni wa kweli na hawataki anayependindishapindisha maneno, na kama kweli wanamtaka Mama Samia, wanamaanisha kwa mila na desturi," alisema Makalla.

Aliwataka kutumia uwezo wa asili kupeleka taarifa maeneo mbalimbali; watangaze habari za CCM ili kishinde kwenye uchaguzi ujao.

"Kuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, lengo la CCM ni kushika dola na ili ushike dola, lazima ushinde uchaguzi, ni lazima mtafute ushindi wa CCM kwa nguvu zote," alielekeza.

Alisema ili CCM ishinde, inahitaji watu wengi na kwamba vitambulisho vya mpigakura havitumiki kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, bali kila mmoja anapaswa kujiandikisha kwenye Daftari la Wakazi katika kila kijiji kuanzia Oktoba 11 hadi 20 mwaka huu.

Alirudia ahadi yake kuwa CCM itawaletea wagombea safi ambao hawana 'makandokando' ambayo ni kero za vijiji ikiwamo kuuza ardhi ya wananchi.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema jeuri yake iko kwenye mikono ya viongozi hao kwa kuwa ndio wanaotafuta kura za Rais, wabunge, madiwani na viongozi wa serikali za mitaa.

Alisema kuna mafanikio makubwa, yakijumuisha ujenzi wa vituo vya afya vitano na vingine vinne vinajengwa mwaka huu wa fedha, huku miradi mingine ya elimu na afya ikitekelezwa.

"Sisi tumeamua fomu ya kugombea urais ya Samia Suluhu Hassan itatolewa na wana Simanjiro, ninakuhakikishia (Makalla) Simanjiro ni ngome ya CCM.

"Tunapoelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ninawahakikishia atakayepata kura halali na kuongoza hata kwa kura moja, hakuna atakayeonewa kwa kukatwa jina, tunataka aliye safi na ambaye rekodi yake ni safi," alisema.

**MADAI KUUZWA ARDHI**

Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, James Ole Milya, alisema kilio kikubwa cha wananchi hao ni ardhi yao ambayo imeuzwa na atalisimamia suala hilo bila kuchoka.

"Ninaomba kamati yangu ya siasa wilaya ituelewe tutakapopitia majina yote yaliyopo, yeyote ambaye aliuza hata ekari moja ya wananchi achukuliwe hatua.

"Sina mahali pa kwenda zaidi ya Simanjiro, CCM itatokana na watu wake ambao ni wakweli. Kama unajua umeuza hata ekari moja ya watu hawa (wana Simanjiro), usiombe fomu ya kuombea," alisema huku akishangiliwa na wananchi hao.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. UTANGULIZI:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi yenye makao yake makuu Morogoro. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Kampasi ya ICoT - Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi katika Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Kumi (10)** 14/10/2024 – 21/12/2024 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**
Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads): Washiriki watajifunza mada mbali mbali kuhusu mbinu za ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Aidha, watajifunza mada mtambuka ambazo zitahusu utaratibu wa namna ya kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara pamoja na Usimamizi wa kazi za Barabara.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**
Masomo katika kozi hii yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani '(Routine/Reccurent), Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za Udongo/Changarawe na Barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**
a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estate Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**
Lugha itakayo tumika katika Kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**
Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo

i. Mshiriki atapata huduma ya chakula na malazi zitolewazo na Taasisi atalipa ada kiasi cha Tsh. 1,600,000.

Ada ya ushiriki ilipwe kwa kutumia 'Control Number' itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi hii watatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa hapa chini ili kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**

**MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ICoT,**

S.L.P 963, MOROGORO.
Simu : 023- 2935229/023- 2935226
: 0762 409087/0787059555/0786 384 062
Nukushi : 023-2935227
Barua pepe : mwti@morogoro.net

S.L.P 1957, MBEYA.
Simu : 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404/0765251509
Nukushi : 025 295 7486
Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com

# 1,158,862 kufanya mtihani kumaliza elimu ya msingi leo

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA) limetangaza kuanza kwa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2024 utaofanyika kwa siku mbili kuanzia leo, huku wadau wa sekta ya elimu wakitakiwa kutoa taarifa za undanganyifu wa aina yoyote.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Ally Mohamed, akizungumza jana mkoani Dar es Salaam na waandishi wa habari kuhusu mtihani huo, aliwataka wenye taarifa za udanganyifu walijulishe Baraza kwa namba 0759 360 000 au barua pepe esnecta@necta.go.tz.

Dk. Mohamed alisema katika mtihani huo, jumla ya watahiniwa waliosajiliwa ni 1,230,780 na kati yao wavulana ni 564,176 sawa na asilimia 45.84 na wasichana ni 666.604 sawa na asilimia 54.16.

"Kati ya 1,230,780 waliosajiliwa kufanya mtihani mwaka 2024, watahiniwa 1,158,862 sawa na asilimia 94.16 watafanya mtihani kwa Lugha ya Kiswahili na 71,918 sawa na asilimia 5.84 watafanya kwa Lugha ya Kiingereza ambayo wamekuwa wakiitumia katika kujifunzia," alisema.

Alisema watahiniwa wenye mahitaji maalumu waliosajiliwa ni 4,583, kati yao 98 ni wasioona, 1,402 wenye uoni hafifu, 1,067 wenye uziwi, 486 ni wenye ulemavu wa akili na 1,530 ni wenye ulemavu wa viungo.

Dk. Mohamed alisema jumla ya masomo sita yatatahiniwa katika mtihani huo ambayo ni Kiswahili, English Language, Sayansi na Teknolojia/ Science and Technology, Hisabati, Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi na Uraia na Maarifa.

"Pamoja na maandalizi yote muhimu yaliyofanyika, Kamati za Mitihani za Mikoa na Halmashauri zihakikishe kuwa usalama wa vituo vya mitihani unaimarika na kwamba, vinatumika kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na Baraza.

"Wasimamizi wahakikishe wanafanya kazi yao kwa weledi na kwa kuzingatia kanuni za mitihani na miongozo waliyopewa ili kila mtahiniwa apate haki yake," alisema.

Dk. Mohamed alisema Baraza halitarajii kuona mwanafunzi yeyote kujihusisha na vitendo vya udanganyifu.

Alisema mwanafunzi atakayebainika kufanya hivyo, matokeo yake yatafutwa kwa mujibu wa kanuni za mitihani.

Katibu Mtendaji ametoa wito kwa wamiliki wa shule kutambua kuwa shule zao ni vituo maalum vya mitihani na hivyo hawatakiwi kwa namna yoyote kuingilia majukumu ya wasimamizi wa mitihani na kwa wakuu wa shule kuzingatia mwongozo wa usimamizi uliotolewa na Baraza kwa kuepuka kuingilia usimamizi wa watahiniwa ndani ya vyumba vya mitihani.

"Baraza linatoa wito kwa jamii kutoa ushirikiano na kuombwa kuheshimu eneo la mitihani kwa kuhakikisha hakuna mtu yeyote asiyehusika na mitihani kuingia katika eneo la shule katika kipindi chote cha mitihani," alisema.

# Serikali kuendeleza ushirikiano huduma ya afya sekta binafsi

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na watoa huduma binafsi wa afya nchini kutokana na mchango wao kuhitajika, husussan katika utoaji matibabu kwa Watanzania.

Kadhalika, imesisitiza azma yake ya kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za afya kupitia Afya Kwa Wote, kwa kuhakikisha unaanzishwa uhakiki wa dole gumba, kabla ya mgonjwa kupatiwa huduma.

Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, aliyasema hayo jana, Dar es Salaam, wakati alipofanya ziara katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, akiambatana na viongozi wengine kutoka wizarani pamoja na Mwenyekiti wa Bodi MNH, Dk. Ellen Senkoro.

Alisema serikali inatambia mchango wa sekta binafsi kwa kushirikiana maeneo muhimu ili wananchi wafikiwe na huduma za afya.

"Sekta binafsi ni lazima isimamiwe, serikali itatoka huduma kwanza, lakini sekta binafsi itasaidia kuongeza nguvu. Na kila aliyepewa jukumu awajibike. Lazima tuwe waratibu wa huduma hizi na tuwasimamie sekta binafsi," alisema Jenista.


Aliongeza kwamba miongoni mwa mafanikio ya sekta ya afya nchini ni kuboresha kwa matibabu na kuwa ya kibobezi na kibingwa, huku MNH ikifikia huduma mbalimbali zenye ubingwa 35 zilitolewa na wataalamu wazawa na hata kushirikiana na wadau wa nje.

"Lazima tukimbizane na teknolojia na sekta hii ikakua na kuwa ya mfano. Huduma za bima ya afya wakati tukielekea huduma ya Afya Kwa Wote tunaweza kuwa na mfumo wa 'biometric' ili kujua nani katibiwa nini, dawa gani kapata, yaani tunataka mifumo isomane," aliongeza waziri huyo.

Vilevile, Jenista alisema serikali itahakikisha ina uimarisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. (NHIF) na kuufanya kuwa endelevu kwa lengo la kuwafikia Watanzania wote.

Dk. Senkoro alimshukuru waziri kwa kutembelea hospitali hiyo, na kwamba yapo mafanikio na changamoto zinazowakabili ambazo wataziwasilisha kwake.

"Bodi tupo mstari wa mbele katika kuyatafsiri maono yako na serikali pia na tutatoa ushauri na kufuata maelekezo yatakayotolewa," alisema Dk. Senkoro.



# Meno ya tembo yawatupa wawili jela miaka 22

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, imewahukumu watu wawili kwenda jela miaka 22 kila mmoja baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kukutwa na vipande vinane vya meno ya tembo.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, alisema kuwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo kinyume na Kifungu cha 86 (1) na (2) (b) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283 iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2022, ikisomwa pamoja na Sheria ya Uhujumu Uchumi Aya ya 14, Kifungu cha 57 (1) na Kifungu cha 60 (2), Sura ya 200 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Waliotiwa hatiani ni Richard Lutama (49), na Mosses Cosmas (28), mkazi wa Babati. Washtakiwa walikuwa wakikabiliwa na kesi hiyo ya uhujumu uchumi, namba 15241 ya mwaka huu. Katika hukumu yake, Hakimu Kimario, alisema washtakiwa walitenda kosa hilo Mei 21 mwaka huu, ambapo walikutwa nyumba ya kulala wageni chumba namba 108 iliyopo kwenye Mjini Babati, wakiwa wameficha vipande hivyo uvunguni mwa kitanda.

**Katika hukumu yake, Hakimu Kimario, alisema washtakiwa walitenda kosa hilo Mei 21 mwaka huu, ambapo walikutwa nyumba ya kulala wageni chumba namba 108...**

Aidha, alisema thamani ya tembo hao ni Dola za Marekani 60,000, sawa na Sh. milioni 154.656.

Hakimu Kimario, alisema upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi wanne na vielelezo sita vilivyofikishwa mahakamani, huku upande wa utetezi walikuwa wanajitetea washtakiwa wenyewe.

Vilevile, alisema baada ya kufanyika upekuzi katika nyumba ya kulala wageni na kuwakuta na meno hayo, kielelezo husika kilipelekwa Kituo Kikuu cha Polisi Babati na ndicho kilichotumika mahakamani.

Awali, Wakili wa Serikali, Berenadetha Mosha, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa washtakiwa kutokana na vitendo vya ujangili kusababisha serikali kupata hasara na kupoteza mapato.



Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA), John Bina (kushoto), akikaribishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Justin Nyari, wakati wa ziara yake ya kuwatembelea wachimbaji madini wa Kanda ya Kaskazini, Mirerani, wilayani Simanjiro, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# TASAF yataja malengo mpango wa pili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKURUGENZI Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shedrack Mziray, amesema utafiti wa mwisho wa kutathmini Mpango wa Pili wa Kunusuru Kaya Maskini wa Mwaka 2024/2025 unalenga kuangalia namna uwekezaji wa serikali unavyoleta tija katika kufikia malengo yaliyowekwa ya vita dhidi ya umaskini.

Amesema kazi ya kutathmini mpango huo inafanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS), kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB).

Alisema hayo juzi mkoani Kilimanjaro wakati wa uzinduzi wa mafunzo yaliyowahusisha wasimamizi na wadadisi kutoka NBS.

Mziray alisema utafiti huo vilevile unaangalia namna ambavyo uwekezaji wa serikali katika kuwahudumia wananchi wake, unavyoweza kuwaondoa katika hali duni na hivyo kuweza kuboresha maisha yao.

Alisema lengo kuu la utafiti huu ni kufanya tathmini katika kaya zinazonufaika na mpango huo kwa Tanzania Bara na Zanzibar; kwa kukusanya taarifa kutoka katika kaya binafsi zinazohusu taarifa za elimu, afya, uwezeshaji wa wanawake, matumizi ya chakula, usalama wa chakula na namna ya kukabiliana na majanga katika kaya.

Alitaja lengo lingine ni kutathmini makazi na rasilimali za kaya, shughuli za kaya zisizo za kilimo, akiba na mikopo, kazi na matumizi ya muda.

Zingine ni shughuli za kilimo, mifugo, malipo kwa njia ya kielectroniki, utekelezaji wa mpango, uwezeshaji wanawake, ustawi wa jamii na unyanyasaji wa kijinsia.

"Tathmini kama hizi ni muhimu sana kwa serikali, kwa sababu zinaelekeza namna ya kuboresha sera kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Jambo hili linathibitishwa na matokeo ya tathmini ya kipindi cha kwanza cha mpango wa kunusuru kaya maskini, ambayo ilionesha walengwa wanapata mahitaji ya msingi yakiwamo chakula na vifaa vya shule kwa watoto," alisema.

Alisema mahudhurio ya watoto shuleni yameongezeka na viwango vya ufaulu katika masomo vimepanda na wanafunzi wanaotoka kaya duni kuchaguliwa katika vyuo vya elimu ya juu.

Alisema: "Wazazi wanapeleka watoto kliniki kwa ajili ya chanjo na ushauri wa kitaalamu katika lishe na malezi. Taarifa zinaonyesha viwango vya lishe kuwa bora zaidi hususani kwa watoto chini ya miaka mitano."

Mziray alisema kaya nyingi zimejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na kupunguza vifo ambavyo awali vilikuwa vikitokea kwa sababu ya watu kushindwa kumudu gharama za matibabu.

# Uzalishaji mboga wavutia vijana Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SEKTA ndogo ya uzalishaji wa mboga mkoani Kilimanjaro imeanza kuwavutia makundi mbalimbali ya vijana kujihusisha na shughuli za uzalishaji kwa njia ya kilimo ikolojia, huku ikionyesha matumaini ya kutengeneza fursa nyingi za maendeleo na ajira.

Mratibu wa Programu ya Kilimo na Mifugo wa Shirika la Floresta Tanzania, linalotekeleza mradi wa AID-I, Sinyati Ng'ida, alisema kilimo hicho kinadhibiti afya ya udongo na ni mojawapo ya njia rahisi na mwafaka zaidi kwa wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao na faida, huku wakiboresha mazingira.

"Kilimo ikolojia tunachohamasisha katika wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro, hasa uzalishaji wa mboga, kinalenga kuongeza bioanuai. Mathalani kinasaidia kuvunja mzunguko wa magonjwa, kuchochea ukuaji wa mimea na kutoa makazi kwa wachavushaji na viumbe wanaoishi kwenye udongo," alisema.

Alisema mpaka sasa wamefanikiwa kutoa elimu kwa vikundi vya kuweka na kukopa vijijini kwa Mkoa wa Kilimanjaro, lakini wamefanikiwa kutoa elimu kwa wanafunzi, walimu na vikundi vinavyotoa huduma ya kuuza chakula.

Zaidi aliongeza: "Lakini kusaidia wakulima wetu waweze kuwa na mfumo mzuri wa mbegu kuanzia uzalishaji mpaka uhifadhi wa mbegu zao binafsi."

Alisema mradi huo unaolenga kuwafikia watu 5,000, unatekelezwa na Shirika la Floresta Tanzania kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Mboga na Uhifadhi wa Mbegu.

Alisema mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID).

Mmoja wa wakulima wa mboga katika Kijiji cha Embukoi, Kata ya Donyomoruwa, Wilaya ya Siha, Maria Mollel, alieleza namna wanavyonufaika kuongeza kipato kupitia kilimo hicho.

Alisema: "Tunaishukuru Floresta Tanzania kwa kutupa elimu hii, inatusaidia wanawake katika kuongeza lishe ya familia na kuongeza kipato cha jamii, hususani wanawake wa jamii ya Kimasai, ambao wako nyuma katika sekta ya biashara."

Mwenyekiti wa Viongozi wa Mila (Leigwanani) wa jamii ya kifugaji ya Kimasai katika Kata ya Donyomoruwa, Lekishon Mollel, alisema mradi huo una manufaa makubwa kwa jamii hiyo kuboresha lishe, kwa kuwa awali Wamasai walikuwa hawali mboga za majani.



# Bil. 77/- kutoa maji Ziwa Victoria hadi Biharamulo

**Na Daniel Limbe,** BIHARAMULO

ZAIDI ya Sh. bilioni 77 zimetengwa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa usambazaji maji kutoka Ziwa Victoria hadi wilayani Biharamulo, lengo likiwa ni kumaliza adha ya upatikanaji wa maji.

Hayo yamebainishwa juzi na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Biharamulo (BUWSA), Siraji Basiga, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake juu ya malalamiko ya upatikanaji maji wilayani humo.

Alisema malalamiko ya wananchi yanatokana na uwezo mdogo wa miundombinu na uchakavu wa mitambo ya kusambaza maji ambao ulisanifiwa miaka 1970, idadi ya wananchi ikiwa ndogo.

Alisema hali hiyo imesababisha serikali kuja na uamuzi wa kujenga mradi huo mkubwa, lengo likiwa ni adha ya muda mrefu ya upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi ambao baadhi yao wamekuwa wakidai kutumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kwenda kuzalisha uchumi wa kaya na taifa kwa ujumla.

"Sasa hivi tunaendelea na ujenzi wa matangi mengine ili kuhakikisha tunapunguza tatizo hilo ambapo mahitaji ni makubwa ukilinganisha na hali ilivyo," alisema Basiga. Alisema tayari wameanza usanifu utakaochukua maji kutoka wilayani Chato mkoani Geita hadi Biharamulo na ndiyo utakuwa mwarobaini wa changamoto zilizopo kwa sasa kwa madai kuwa kutakuwa na maji ya kutosha.

"Hatua mbalimbali zinakamilishwa ili kutangaza tenda hiyo ambayo itasimamiwa na Mamlaka ya Maji Mkoa wa Kagera kwa lengo la kuhakikisha unakuwa na ufanisi mkubwa kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo," alisema Basiga.

Baadhi ya wakazi wa Biharamulo, Atusime Albogast walisema upatikanaji wa maji kwa sasa siyo wa kuridhisha kwani yanapatikana kwa saa 12 pekee.

# Maofisa ugani walia kukosa mafuta ya pikipiki

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MAOFISA ugani wilayani Sengerema mkoani Mwanza wamesema licha ya kupatiwa pikipiki kwa ajili ya kuwafikia wakulima kwa wakati wanashindwa kufanya hivyo kutokana na kutokuwa na mafuta.

Walitoa malalamiko hayo juzi mbele ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Zacharia Mwita wakati wakikabidhiwa vishikwambi kwa ajili ya kuwasaidia kutoa elimu ya kilimo cha kisasa kwa wakulima.

Mmoja wa maofisa ugani, Zacharia Mwita alisema: "Hili ndilo tatizo kubwa linalotukabili kwa sasa na kusababisha kutokufika kwenye mashamba ya wakulima kwa wakati, hivyo tunaomba kupewa mafuta ili tuweze kufanya kazi katika mazingira yoyote".

Akijibu ombi hilo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Yanga Makanga alisema watawawekea mafuta ili kuwawezesha katika kazi zao na kuweza kuwafikia wakulima muda wowote.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vishikwambi hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, aliwaonya maofisa ugani wanaokaa nje ya vituo vyao vya kazi wakati wa kutoa huduma bila sababu maalum.

Alisema hali hiyo inasababisha wakulima kukosa msaada wa haraka pindi wanapofika katika ofisi zao.

Alisema hali ya maofisa kuwa mbali na vituo vyao inawafanya wakulima wanaohitaji huduma ya dharura kushindwa kuipata kwa wakati, kuwasababishia wakulima kukata tamaa, na kuleta mavuno kidogo.

Aidha, aliwataka kutumia vishikwambi hivyo kwa matumizi yalipangwa na siyo kwa matumizi mengine.

Pia, aliwataka kutumia matumizi mengine pamoja na kuzingatia utaratibu wa vifaa kutunza vitendea kazi na kufanya kazi kwa bidii.

"Kasimamieni vyema wakulima ili wilaya iwe na chakula cha kutosha, tuache kuomba chakula nje ya wilaya kwani kukiwa na utoshelevu wa chakula hapatakuwa na haja ya kuomba chakula nje," alisema Ngaga.



Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Wazee, wilayani Kishapu, Suzana Masebu, akiwasilisha mapendekezo na mahitaji ya wazee wilayani humo juzi, kwa Katibu wa Mbunge wa Kishapu, Godfrey Mbussa, kwa niaba ya Mbunge Boniphace Butondo, ili awasilishe kwenye ngazi za juu, ambapo miongoni mwa mapendekezo ni pamoja na kutungwa kwa sheria ya wazee na kuboreshewa huduma za afya. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wafanyabiashara waitwa kusajili biashara BRELA

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umewaita wafanyabiashara pamoja na wamiliki wa kampuni kufika katika Maonesho ya 19 ya Afrika Mashariki ili kupata huduma za papo kwa papo za kusajili majina ya biashara, kampuni pamoja na elimu ya usajili leseni na shughuli za wakala huo.

Wito huo umetolewa jana na Msaidizi wa Usajili BRELA, Selemani Selemani, wakati wa utoaji wa huduma katika banda la taasisi hiyo lililopo kwenye maonesho hayo yanayofanyika katika viwanja vya Furahisha mkoani Mwanza.

"Wajasiriamali pamoja na wafanyabiashara wakubwa tunaendelea kuwapatia elimu katika maonesho haya ambapo tupo tangu Septemba, 6 mpaka 15, hivyo tunawakaribisha waendelee kuja ili kupata elimu juu ya faida za usajili wa majina ya biashara pamoja na kutoa huduma zote," alisema.

Alisema kwa wale wanaokutana na changamoto ya kimfumo katika kupata huduma wafike ili kupatiwa huduma hizo kwa haraka zaidi.

Alisema: "Wafanyabiashara wote wasikubali kufanya biashara kimyakimya waje katika banda letu wafanye usajili, wapate na elimu ya usajili za majina ya biashara pamoja na kampuni," alisema.

Mmoja wa waliopata huduma pamoja na elimu kupitia wakala huo, Emmanuel Lukas, alisema amefika kwa ajili ya kusajili kampuni na kupokea elimu ya usajili pamoja na vitu vinavyohitajika, hivyo aliahidi kurejea siku inayofuata.

# Wazee wamkumbusha Waziri Mkuu ahadi aliyoitoa

**Na Marco Maduhu,** KICHAPU

MWENYEKITI wa Baraza la Ushauri la Wazee wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, Suzana Masebu, amesema wazee wanahitaji Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 ihuishwe na kutungiwa sheria itakayokuwa na nguvu ya kiutekelezaji katika masuala yanayowahusu.

Kadhalika wazee hao wamemkumbusha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kutekeleza ahadi yake aliyoitoa katika Siku ya Wazee Duniani ambayo kitaifa ilifanyika mkoani Mtwara mwaka 2019 kwamba itatungwa Sheria ya Wazee.

Walibainisha hayo juzi wakati wakiwasilisha mapendekezo na mahitaji yao kwa mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo aliyewakilishwa na katibu wake ili yafanyiwe kazi yaliyo ndani ya uwezo wake pamoja na mengine ayawasilishe ngazi za juu.

Alitaja mapendekezo mengine kuwa wazee wanahitaji wawe na pensheni ya kuwasaidia kila mwezi kwa kiasi chochote cha fedha ili wajikimu, kwa sababu wazee wachache wapo kwenye mfumo rasmi na wengine hawapo kwenye mfumo huo.


Ofisa ufuatiliaji wa masuala ya wazee kutoka Baraza la Ushauri la Wazee Shinyanga, Lurent Mihayo, alisema wanakutana na wabunge wote wa mkoa huo ili kuwasilisha mapendekezo na mahitaji ya wazee kwa kila halmashauri yafanyiwe kazi.

Katibu wa mbunge wa jimbo hilo, Godfrey Mbussa, alisema mapendekezo na mahitaji hayo yamefika sehemu husika kwa sababu mbunge ni mwakilishi wa wananchi na atayafanyia kazi.



Ukurasa 13

**LINAVYOAKISI UTAYARI WA CHINA KUIPA AFRIKA VIWANGO VINGINE**




Ukurasa 14

**'China ilivyo mbeleko sahihi kuibeba Afrika'**



# Kujua ufumbuzi wa shida kitaalamu ni mbadala wa wahubiri kiboko ya uchawi

**Na Godfrey Julius, UDSM**

WAKATI binadamu wanapokabiliwa na matatizo ulitarajiwa kuwa muda wa kuyatafakari kwa kina ili kupata ufumbuzi, lakini badala ya kusaka suluhisho, njia nyepesi zama hizi wengi ni kukimbilia kwa waganga na kwa viongozi wa dini.

Waganga hao ni wa ramli, kadhalika wahubiri ni wale wanaofundisha injili iliyoghoshiwa au kuchakachuliwa ili kukidhi wanachotomani walimu hao wa imani.

Zama hizi kumeibuka nyumba za ibada kwenye maeneo mengi hasa mijini wahubiri wakitanguliza majina na vyeo vyao, wako wanaojiita mitume hata manabii, jambo linalokua kila siku.

Ni jambo la kushangaza kwamba watu wengi wanapishana malangoni kwa wahubiri kupata ufumbuzi wa matatizo na changamoto zinazowakabili, sheria haziwazuii lakini wanatakiwa kujiongeza.

Inawezekana kuna matatizo mengine yanayozaliwa kwa wahubiri hao pasipo wenyewe kufahamu, mfano kufilisika kwa kutozwa sadaka kubwa, kulazimishwa kuacha shughuli za kiuchumi, chuki wanafamilia wakidaiwa ni wachawi na wakwamishaji.

Hivi karibuni Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, alikemea suala hilo akisema yameibuka mafundisho ya kuwahamasisha watu kwenda kwenye nyumba za ibada kuombewa ili wapate mali ikiwamo nyumba, fedha, na kutatuliwa shida zao.

"Tunashuhudia kuongezeka kwa wahubiri wanaojilimbikizia fedha na mali binafsi kutokana na sadaka na mauzo ya vitu mbalimbali vya hao watu wanyonge."

Anasema: "Na wahanga wengi wa mahubiri ya aina hiyo ni watu wanyonge wanaokabiliwa na matatizo mengi kama umasikini, migogoro ya ndoa, ugumba na kukosa ajira."

Ni muda sahihi kuamka kutoka kwenye usingizi wa pono na kijiepusha na utapeli mpya ambao unaendelea kushika kasi kupitia dini tena ukidaiwa kufanywa ndani ya nyumba za ibada.

Inashangaza watu kujinadi kuwa wametumwa na mungu wakitamba moja kwa moja. Wanajigamba kutatua shida na changamoto zinazowakabili wanadamu duniani hapa.

Wenye udhaifu wapokee miujiza ya uponyaji, wasio na ndoa wapate wenza na hata wale waliofiwa na ndugu na jamaa zao waweze kufufuliwa na kuishi tena.

Mafundisho haya yamewafanya wengi kuamini kuwa wanaweza kupata utatuzi na ufumbuzi wa matatizo yao mathalani kuongeza wateja katika biashara, kuboresha ndoa, kupona magonjwa, kuwa matajiri, ahueni katika migogoro ya kifamilia na ajira.

Pamoja na kwamba watu hawa huenda wakiwa na matarajio makubwa ya kupata ahueni ya matatizo yao, lakini wanaendelea kuibiwa na kutapeliwa sadaka na fedha za viingilio vya kuonana na wahubiri hao waongo.

Kuna haja ya serikali kuja na mikakati madhubuti ya kuwachunguza watu hawa hususan aina ya mafundisho wanayofundisha ndani ya nyumba za ibada.

Wengi wao wanatumia mwanya huo wa kuhubiri Neno la Mungu kama sehemu ya kuwarubuni na kuwaibia Watanzania ambao ni waamini. Hata hivyo, hukutana na masharti na maagizo magumu kutoka kwa viongozi hao wa dini.

Kwa mfano ili kuwafanya waamini hao watoe fedha za kutosha kumewekwa hadi viingilio, kiasi cha kudhani kwamba unalipia kiingilio katika Uwanja wa Benjamini Mkapa kwenda kuzishuhudia Simba na Yanga zikichuana kumbe sivyo.



Mchungaji Dominic Kashoix au Dibwe, aliyefungiwa kanisa kwa madai ya kukiuka maadili. **PICHA: MTANDAO**

Wakumbuke Neno la Mungu lenyewe linawaagiza wahubiri "kutoa bure" kwa kuwa karama hizo "wamezipata bure" kutoka kwa Mungu.

Waamini wanauziwa maji, mafuta, vitambaa hata na udongo na kuombewa kwa gharama kubwa hali inayosababisha hata vipato vyao kurudi nyuma tofauti na walivyodhani.

Inawafanya wengine kuhisi kuwa ni mwisho wa dunia kama ulivyotabiriwa katika vitabu vitakatifu, kutokana na hayo yaliyonenwa na kutabiriwa hasa kupenda pesa na kumwacha Mungu.

Kwa kiasi kikubwa mafundisho ya sasa yanavuka mipaka ya kimaadili na mengine yanahamasisha chuki na uchochezi. Ikumbukwe mwishoni mwa Julai, Kanisa la Christian Life Church huko Buza jijini Dar es Salaam chini ya Nabii Dominiki Dibwa au 'kiboko ya wachawi.'

Mhubiri huyo raia wa DRC anatoa mafundisho ambayo ni ya kiudhalilishaji na unyanyapaaji, madai yalitolewa hatua iliyofuatiwa na kupokea barua ya serikalini ya kumtaka asitishe shughuli zake za kidini mahali hapo kutokana na kile kilichodaiwa kuwa mafundisho yake yanakiuka maadili ya Kitanzania ikiwamo uchonganishi.

Aidha, alidaiwa kuwafundisha waamini wake kuua watu. Pia, sababu nyingine iliyotajwa kusababisha mgogoro kati ya nabii huyo na serikali ni kuwatoza waumini wake Shilingi 500,000 pale walipohitaji kuombewa, jambo ambalo ni kinyume cha maadili ya kidini. Hata hivyo, siku chache baadaye aliondoka nchini na kurejea DRC.

Ili kutoa ushuhuda na kuthibitisha kuwa Watanzania walikuwa wakiibiwa na kurubuniwa pesa zao, akiwa DRC anaonekana katika vipande kadhaa vya picha jongefu akiwakejeli Watanzania, mathalani wale waliokuwa wakimpatia fedha kwa ajili ya kuwafanyia maombi.

Nabii Dibwe hivi sasa amevuka mipaka kiasi cha kutoa maneno machafu kwa wale waliokuwa wakitoa fedha hizo kwa ajili ya kufanyiwa maombezi kuwa ni "wendawazimu". Je, hii ni sawa? Na vipi kuhusu hawa manabii na mitume wengine ambao wanaendelea kutoa huduma maeneo mengine? Ni taswira gani inapatikana? Je, hakuna wengine walio na madhumuni kama ya huyu "Kiboko ya Wachawi?"

Watanzania tumakinike na hili, tujikite katika kuchakata bongo zetu ili tujue matatizo yetu yanasababishwa na nini, na si kudhani kwamba biashara zetu zisipoenda vizuri basi tumerogwa. Ama eti mahusino yetu yakivunjika, kimbilio ni kwa nabii pekee penye suluhisho kamili.

Mambo haya yanayoendelea hivi sasa hasa kupitia mikasa hii ya manabii, mitume na makuhani, yawe ni sehemu ya kutoa fundisho kwa watu wote wanaotumia fedha zao nyingi kwa manabii na mitume kwa lengo la kutaka kupata ufumbuzi wa matatizo yao ilihali matatizo yao yanabakia kuwa palepale.

Watanzania waachane na kua-

INAENDELEA UK. 12

# Matukio kuteka, kuua ni ukakasi kufikia R4 za Rais

**Na Mwandishi Wetu**

UJENZI wa taifa unahitaji mchango wa kila Mtanzania bila kujali tofauti za kisiasa, dini, jinsi na ukanda.

Kwa kuzingatia hilo, Rais Samia Suluhu Hassan, anasisitiza umoja wa kitaifa ili Watanzania washiriki kwa uhuru katika ujenzi wa nchi yao kupitia maarifa, mawazo, elimu na shughuli za kiuchumi wafanyazo.

Akiona umuhimu huo wa ujenzi wa taifa kwa pamoja, Rais anasimamia falsafa ya R4 ambazo zinatafsiriwa Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahimilivu), Reform (Mabadiliko) na Rebuiding (Kujenga upya).

Maridhiano ni muhimu katika ujenzi wa taifa ili kuwa na sauti moja, kwani maelewano yanawezesha kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa umoja, amani na kukosoana.

Hata hivyo, baadhi ya wanasiasa wanasema, falsafa hiyo ya Rais inaweza isifanikiwe iwapo matukio ya yanayoendelea sasa ya utekaji wa watu na mauaji vitaendelea bila kuchukuliwa hatua madhubuti ya kuvidhibiti.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha CUF Bara, Magdalena Sakaya anasema, yanayotokea sasa ni kama hizo 4R za Rais hazina maana.

"Matukio haya ni kwamba kuna kadhaa ninayoyaona. Kwanza Rais, hajagundua kinachoendelea au kuna watu wanamzunguka ama kuna watu ndani ya serikali wanamzunguka," anasema Magdalena.

Naibu katibu mkuu huyo anasema, ni wakati sasa Rais kusimamia 4R zake kwa vitendo, kwa maelezo kwamba inawawia vigumu Watanzania kujua ni nani anaagiza matukio ya utekaji na kuua watu.

"CUF tumepokea kwa mshtuko taarifa ya kuuawa kwa Mjumbe wa Sekretarieti Kuu ya (CHADEMA), Ali Mohamed Kibao. Matukio ya watu kupotea na kukutwa wameuawa yanaanza kujirudia," anasema.

Anasema, Rais ana nia ya kweli ndio maana alianzisha falsafa hiyo na kuunda Tume ya Haki Jinai, inayogusa haki ya kwanza binadamu ambayo ni kuishi, na kwamba anashangaa kuona yanakuwapo matukio yanayokwenda kinyume na falsafa na haki ya kuishi.

Anatoa wito kwa serikali kushughulikia tatizo hilo ambalo anasema linatengeneza hofu na kuirudisha nchi katika maisha ya taharuki na kuwafanya watu kuishi pamoja kwa upendo na kuaminiana.

### AIBU KWA TAIFA

Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, anasema, matukio hayo ni aibu kwa taifa lenye amani na utulivu na ni kikwazo kwa falasa ya Rais.

"Tumemsikia Rais akisema anataka taarifa za matukio hayo haraka, nasi tunaomba uchaguzi usizidi wiki mbili, ikiwezekana, waitwe wachunguzi wa kimataifa kama CIA ya Marekani kusaidia kuchunguza," anashauri Ngwaiya.

Anafafanua kuwa vyombo vya uchunguzi vya Tanzania vipo, lakini matukio yanazidi kuongezeka na kuongeza kuwa njia nzuri ni kuongeza wachunguzi kutoka nje ili ukweli ujulikane.

Mwenyekiti huyo anasema, uchunguzi ukikamilika, watangazwe hadharani ili watu wawajue na iwe fundisho kwa wengine ambao wamekuwa wakiteka watu na kuchafua taswira ya nchi na kusababisha hata wageni kuwa na mashaka usalama wa maisha yao wawapo nchini.

"Kuishi ni haki ya kikatiba ya kila mtu, hakuna mtu mwenye ruhusa ya kutoa uhai wa mwingine. Sisi CEGODETA tunafuatilia ili kuona haki inatendeka, asiwepo wa kuonewa katika uchunguzi huo, na ni vyema ukafanyika kwa muda wa wiki mbili," anasema.

### UPINZANI KWA RAIS

Kada wa CCM ambaye ni mchambuzi wa siasa, Abdulkarim Atiki, anasema, matukio ya kuteka na kuua watu yanafanywa na wale wanaopinga falfasa ya Rais Samia.

"Hao ni wale wanaoendekeza siasa za ubabe tulizoshuhudia zaidi ya miaka sita iliyopita, Rais amejitahidi kuwaunganisha Watanzania, lakini anakutana na upinzani," anaonya Atiki.

Anasema, mtu akitaka kutenda haki kwa wananchi ni lazima atakutana na upinzani, na kwamba hata Rais anakutana nao kwa njia hiyo ya matukio ambayo inalenga kumchafua mbele ya jamii.

Anafafanua kuwa kiongozi wa nchi anataka mgombea anayeshinda katika uchaguzi apewe haki yake, na kwamba ndio maana ameruhusu kuwapo Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

"Ukiniuliza kuhusu matukio yanayoendelea, nitayaita upinzani kwa Rais unaofanywa na wasiomtakia mema, lakini ninamtia moyo aendelee kuchapa kazi kuunganisha Watanzania," anasema.

Mchambuzi huyo wa siasa anasema, uongozi wa Rais Samia umepoza machungu ambayo Watanzania walikuwa nayo kuanzia mwaka 2015 hadi mwanzoni mwa mwaka 2021, wakati wa awamu ya tano.

"Katika siasa, wapo baadhi ya watu wana mihemko, hawa wanatakiwa kupelekwa katika vyuo maalum ili wakafundishwe jinsi nchi inavyoongozwa, badala ya kuonyesha ubabe.

### UKIMYA NI CHANZO

Mwanachama wa CHADEMA, Suzan Lyimo anasema, ukimya wa vyombo vya dola ni chanzo cha matukio hayo na kufafanua kuwa falsafa ya R4 na kuifanya ikose maana kama matukio hayo ndani ya jamii.

"Kuna kauli zilizowahi kutolewa na baadhi ya makada wa CCM za kutishia kupoteza watu, lakini viongozi wa chama hicho walisikika wakiwakana, lakini vyombo vya dola vikawa kimya," anakumbusha Suzan.

Anasema ukimya huo wa vyombo vya dola umetengeneza hofu na kuirudisha nchi enzi za vitisho, taharuki na kila aina ya vitendo vya ukatili ambavyo havikubaki ndani ya jamii iliostaarabika.

"Ni vyema Rais akajitokeza mwenyewe na kuzungumza na vyombo vya habari kuhusu matukio hayo ambayo yanaenda kinyume na falsafa yake ambayo inalenga kuwaunganisha Watanzania," anasema.

Suzan anasema, matukio ya kuteka na kuua watu yanapaswa kulaaniwa na watu wote wakiwamo viongozi wa dini, si wanasiasa tu, pia kuhakikisha waliohusika wanakamatwa.



Ally Kibao, mjumbe wa Sekretariati ya CHADEMA Taifa, alishushwa kwenye basi la Tashrif na watu wasiofahamika na mwili wake kuokotwa Ununio wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

> Katika mazungumzo yake na gazeti hili, Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha CUF Bara, Magdalena Sakaya anasema, yanayotokea sasa ni kama hizo 4R za Rais hazina maana.

## KUJUA UFUMBUZI WA SHIDA KITAALAMU NI MBADALA WA WAHUBIRI NENO 'WACHAWI'

**INATOKA UK. 11**

mini uchawi na ushirikina au kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kupata maombezi kwa viongozi hawa wa dini. Pia, mara kadhaa zimesikika shuhuda za watu waliosafiri umbali mrefu kwenda kuhudhuria ibada kubwa za manabii na mitume zilizopambwa kwa majina mazuri na makubwa kiushawishi.

Lakini ibada hizo zilishindwa kutoa suluhisho katika matatizo yao, hata maji, mafuta, maandazi, udongo, vitambaa walivyopewa bado havikuweza kufua dafu badala yake vikawa kama sehemu ya kuongeza hasara ya upotevu wa fedha na muda kwa watu hawa.

Je, hatuoni haja ya kutafuta vyanzo halisi vya matatizo yetu yanayotukabili na kuacha kurundikana kwa manabii, mitume na makuhani? Kwa maana sio kila tatizo lazima litatuliwe na nabii au mtume kama ambavyo watu wengi wanadhani na kufikiri.

Umefika muda ambao Watanzania wanahitaji kupewa elimu ya kutosha ili kunusuru janga hili ambalo halijulikani lilianzia wapi, kadhalika ukomo wake bado ni kitendawili kigumu.

Pia, ipo haja ya serikali kupitia kwa Msajili wa Jumuiya za Kiraia wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kufanya uchunguzi wa kina kuhusiana na asasi zote za kidini na kuhakikisha kuwa zile zilizomo nchini zinakuwa na vibali vinavyohitajika.

Ikumbukwe kuwa, suala la kukidhi vigezo na kuwa na vibali tu halitoshi badala yake mafundisho yote yanayotolewa kwa watu yanapaswa kuchunguzwa, kwani wengi wa manabii na mitume hao wamekuwa wakitoa mafundisho ambayo ni ya kupalilia ujanja na kujipatia mali.

JUKWAA LA FOCAC

# Linavyoakisi utayari wa China kuipa Afrika viwango vingine

• Uwekezaji popote kwenye dawa, kandanda, viwanda



Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia jukwaa la Afrika, China wiki iliyopita. **PICHA: IKULU**

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ni miongoni mwa marais wanaohutubia Jukwaa la Ushirikiano la China na Afrika (FOCAC), linalomalizika Beijing wiki iliyopita.

Mwalimu wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Taaluma za Kimataifa cha Shanghai (SISU), Ning Yi, anazungumzia mkutano huo, akisema kufanyika kwa mara nyingine kwa jukwaa hilo, kumeleta matokeo chanya ya ushirikiano kwa Afrika.

Ning anasema tangu kuanzishwa kwa FOCAC mwaka 2000 imefanyika mikutano mitatu ya jukwaa hilo ngazi ya juu na minane ya mawaziri ambayo matunda yake ni pamoja na kuongezeka zaidi kwa biashara na uwekezaji kati ya China na Afrika.

"China imeendelea kuwa mshirika mkubwa zaidi wa biashara wa Afrika kwa miaka 15 mfululizo, na katika kipindi hicho, kampuni nyingi zinazotoka katika nchi hiyo, zimechangia ajira zaidi ya 1,000,000 barani Afrika, kwa hiyo haya ni matokeo chanya na ni suala ambalo nchi hizo zinapaswa kujivunia," anasema Ning.

"Na wakati ushirikiano baina ya China na Afrika ukiendelea kupanuka na kuimarika, mkutano wa viongozi vijana wa pande hizo mikutano mingine kadhaa imefanyika.

Mfano ule wa 'think tank', wa kiraia, wa ushirikiano wa vyombo vya habari, ushirikiano wa kupunguza umaskini na kukuza maendeleo, wa ushirikiano wa kilimo, wa amani na usalama na majukwaa mengine ya ushirikiano yameanzishwa yakiendeleza ushirikiano mwema na hivi ndivyo vinapaswa kuwa katika kukuza demokrasia na uchumi kwa ushirikiano kwa ajili ya faida kwa pande zote, anasema.

Aidha anasema FOCAC ina manufaa mengi kama kushauriana kwa uwiano sawa, kuongeza uelewa, kupanua wigo wa maelewano, kuimarisha urafiki na ushirikiano pamoja na kupiga hatua ya maendeleo kwa pande zote kati ya China na Afrika.

Anasema huenda baadhi ya washirika hawakulipa nguvu kubwa wakati linaanzishwa lakini kutokana na matunda yanayoonekana sasa tayari kila nchi mshirika anafurahia uwapo wake kwa ajili ya ustawi wa demokrasia na maendeleo.

"Na sasa tunashuhudia jukwaa hili limekuwa kipimo bora cha thamani cha ushirikiano kati ya China na Afrika na limekuwa bendera ya kuongoza ushirikiano wa kina kwa sababu mpaka sasa kuna nchi wanachama wake 55 ambazo zimeanzisha uhusiano wa kidiplomasia, anasema.

Anaongeza kuwa upo umuhimu wa jukwaa hilo kuendelea kuimarishwa na kupewa nguvu zaidi kwa ajili ya ustawi wa kidiplomasia kwa wanachama wake.

Akihutubia mkutano wa FOCAC, Rais Samia, anasema licha ya changamoto ya uchumi wa dunia miaka ya hivi karibuni, China imeendelea kuwa rafiki wa kweli kwa kuhakikisha utekelezaji wa kiwango cha juu cha makubaliano yaliyofikiwa katika mikutano mbalimbali ya FOCAC.

Anasema jukwaa hilo kwa mwaka huu limekuwa la kihistoria kwa kuwa limefanyika baada ya muongo mmoja wa kupitishwa na kuzinduliwa kwa Mkakati wa Afrika na China jijini Dar es Salaam na Rais Xi Jinping , alipofanya ziara ya kwanza barani Afrika mwaka 2013.

Anasema matokeo ya ushirikiano imara na madhubuti kati ya China na Afrika yanadhihirika kupitia maendeleo makubwa ambayo Afrika imeyapata kupitia ushirikiano wa nchi hizo pamoja na kufanyika chachu katika kukuza chumi za nchi nyingi za Afrika pamoja na kuleta maendeleo ya watu kupitia miundombinu na ukuaji wa maendeleo ya viwanda vidogo na vikubwa.

Kadhalika, Rais Samia akishiriki mkutano wa ngazi ya juu kuhusu maendeleo ya viwanda na kilimo cha kisasa akisema licha ya ajenda ya kilimo kuwa ya muda mrefu barani Afrika, lakini kinakosa ukuaji wenye tija, hivyo bara hilo linahitaji kuungwa mkono na nchi zilizoendelea kama China ili kunufaika na kilimo cha kisasa.

Kadhalika anasema Tanzania imeendelea kuweka mkazo kuendeleza sekta ya kilimo na viwanda na mchango wa vijana katika sekta hiyo unaongezeka kupitia programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) ambayo inalenga kuwanashirikisha katika kilimo chenye tija.

> "Aidha anasema FOCAC ina manufaa mengi kama kushauriana kwa uwiano sawa, kuongeza uelewa, kupanua wigo wa maelewano, kuimarisha urafiki na ushirikiano pamoja na kupiga hatua ya maendeleo kwa pande zote kati ya China na Afrika.

Rais Samia anasema jitihada za serikali peke yake hazitoshi, akiialika sekta binafsi ya China kuwekeza Tanzania kwenye mbegu bora, vifaa vya kisasa vya kilimo pamoja na ujenzi skimu za umwagiliaji ili kulima kisasa na kuongeza thamani katika mnyororo mzima wa kilimo.

Akihutubia wakati akifungua FOCAC Rais wa China, Xi Jinping, anaahidi kushirikiana na Afrika katika maeneo anuwai ikiwa ni pamoja na kufuta kodi kwa bidhaa zinazotoka Afrika ambazo tayari zina uhusiano na China.

Rais, Xi Jinping anasema uhusiano wa China na Afrika utazingatia vipaumbele vya maendeleo ili kuhakikisha uchumi jumuishi wa pande hizo za nchi za Afrika inazoshirikiana nazo.

Ahadi nyingine ni pamoja na utayari wa China kuunga mkono nchi zitakazokuwa wenyeji wa mashindano ya Youth Olympics ya mwaka 2026 na mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) ya mwaka 2027.

Anasema China itawekeza kwenye afya, ikiwamo ujenzi wa viwanda vya dawa pamoja na kutoa uzoefu katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

JUKWAA LA VIONGOZI

# 'China ilivyo mbeleko sahihi kuibeba Afrika'

Na Gaudensia Mngumi



Rais wa China, Xi Jinping.

USHIRIKIANO wa China au Beijing na Afrika unazidi kuota mizizi na wiki hii mataifa hayo yanaandika tena historia. Ni baada ya kufanyika mkutano wa tisa unaozileta pamoja China na Afrika, ukimalizika Beijing, maarufu Forum on China-Africa Cooperation (FOCAC).

Ni utaratibu unaoanzishwa mwaka 2020 na hufanyika kila baada ya miaka mitatu.

Ushirikiano wa China na Afrika kwa muda mrefu umekuwa ukikabiliwa na upinzani kutoka kwa wapinzani wa Beijing hasa mataifa ya Magharibi.

Mara nyingi ni Marekani na baadhi ya nchi za Ulaya zikidai kuna upendeleo wa kisiasa unaoinufaisha China zaidi na kuacha mafanikio kidogo kwa nchi za Afrika.

Hata hivyo, Waafrika wanaona kuwa hayo hayana nafasi sasa. Wengi hasa wanaoihurumia Afrika wanashutumu nchi za Magharibi kwa unyanyasaji na unyonyaji, zikiitumia Afrika kama 'urithi wao wa kikoloni' .

Zinaendeleza ukandamizaji kwa njia za kidiplomasia na kichumi kwenye kuendelea kununua malighafi kutoka Afrika bila kuacha alama za maendeleo zinazoonekana.

Ukweli ni kwamba mashirika wakopeshaji wakubwa Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wanashutumiwa kwa kunyonya mataifa ya Afrika kupitia mikopo na masharti magumu.

Hata hivyo uwekezaji wa Beijing umesaidia Afrika kuwa ya kisasa na kutoa maelfu ya ajira kwa vijana.

Kwa Tanzania China inajenga ukanda mkubwa wa uwekezaji wa viwanda Afrika Mashariki na Kati wa SINOTAN unaojengwa Kwala wilayani Kibaha mkoa wa Pwani.

Lakini China imejenga bandari kavu ya Kwala ambayo inaendeleza uboreshaji usafirishaji shehena Afrika Mashariki, Kusini na Kati, ikipunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mwaka jana kampuni ya China ya CHEC, ilijenga na kukarabati mageti saba na kuboresha upakuaji na usafirishaji wa shehena.

China inajenga barabara za mwendokasi jijini Dar es Salaam na kuboresha usafiri lakini pia hata magari yaendayo haraka yanatoka China. Mabasi yaendayo mikoani hasa YUTONG na pikipiki na kwa ujumla vyombo vyote ya usafiri hutoka China vikitumiwa karibu Afrika nzima.

Kadhalika Daraja la Kijazi au interchange ya Ubungo Dar ni matunda ya ushirikiano wa China na Tanzania ambao mara nyingi unabakiza alama zisizofutika na endelevu.

Mtandao wa usafirishaji wa Ethiopia, unasema China imejenga reli ya kisasa ya SGR inayounganisha Addis Ababa, Ethiopia hadi Djibouti, zikiwa ni kilometa 752 zinazohudumia mataifa hayo yasiyo na bandari.

Aidha, China imejenga mradi wa upanuzi wa bandari kavu nchini Ethiopia na kuongeza uchukuzi wa shehena katika nchi hiyo yenye uchumi mkubwa Afrika Mashariki na Afrika pia, unaongeza mtandao huo.

Madai kuwa China inainyonya Afrika yana mantiki kwa mataifa ya Magharibi, kwa sababu yanaona kuwa yamepungukiwa na ushawishi wao barani Afrika.

Anasema Jana de Kluvier, mtafiti wa uhusiano wa China na Afrika katika Taasisi ya Mafunzo ya Usalama yenye makao yake makuu Afrika Kusini (ISS).

Kwa zaidi ya muongo mmoja, China imekuwa mshirika mkubwa zaidi wa kibiashara wa Afrika. Pia ndiye mkopeshaji mkuu wa bara hilo, ikiwapatia zaidi ya Dola za Marekani bilioni 170 iwe mikopo na misaada katika takriban mataifa yote 54 ya Umoja wa Afrika.

Kwa China, faida ziko katika kuongezeka ushawishi wa kidiplomasia ambao ina hakika kuwa na nguvu katika Umoja wa Mataifa.

Aidha, inapata uungwaji mkono na inaweza kukabiliana na wapinzani wake wa Magharibi ikiwamo Marekani, anasema de Kluvier.

Uwekezaji mkubwa wa miundombinu Afrika unaofanywa na China ni utekelezaji wa miradi ya kujenga miundombinu inayoonekana, si kama misaada ya Kimagharibi ambayo mara nyingi si endelevu.

Mradi huo kabambe wa kujenga miundombinu ulioanza 2013 unaolenga kuunganisha China na Asia, Afrika na Ulaya kupitia mtandao wa bandari, reli, madaraja na barabara kuu.

Majiji na miji Afrika yanajivunia reli mpya zinazogharamiwa na China au kujengwa na kampuni zake China, madaraja na barabara kuu. Yote hayo yamefanikisha harakati za kuunganisha nchi nyingi, majiji na miji na kuondoka kutoka reli za zamani za enzi ya ukoloni ambazo kwa kiasi kikubwa zilikuwa zimepitwa na wakati na zisizofanya kazi kwa ufanisi.

Kazi kubwa za ujenzi zimetoa nafasi za kazi kwa vijana kampuni za ujenzi na makandarasi wa ndani.

Mfano Kenya, reli ya kutoka Nairobi hasa Mombasa kwa mara ya kwanza inaunganisha miji hiyo miwili muhimu na kupunguza muda wa safari ya barabara kwa nusu ilikuwa ikitumia saa 10.

Katika mradi huo zaidi ya Wakenya 25,000 waliajiriwa kuikamilisha, takwimu za Wizara ya Ujenzi zinasema.

Mambo hayakuishia hapo nchini Nigeria, Lagos kuna ujenzi wa miundombinu inayounganisha Nigeria na Port Gentil nchini Gabon na kuwezesha kupata bandari za kina kirefu cha bahari.

Kwa upande wa Ethiopia huo ulifanikisha kujengwa ukanda wa viwanda vya kutengeneza nguo wa Hawassa, ni miradi inayokuza uchumi na kuongeza ajira.

China imesonga mbele kwenye mienendo ya ukuaji wa miji wa China, unakua kwa kasi zaidi, ikisemekana kuwa haijawahi kutokea duniani.

China imewaondoa watu milioni 800 raia wake kutoka kwa umaskini katika kipindi cha miaka 40.

Nchi za Kiafrika zinakua kwa kasi zaidi, na Umoja wa Afrika unataka miji mikubwa iunganishwe kwa reli ifikapo 2063 na kazi inayotarajiwa kufanywa na China.

China ni mshirika mkubwa wa maendeleo ya Afrika kwenye ajenda ya 'Afrika Tunayoitaka . The Afrika we want agenda 2063' .

Matokeo ya uwekezaji ya China yanaonekana Afrika kwa sababu ni ya haraka na yanatekelezeka kuliko ahadi za nchi za Magharibi.

China kwa kifupi misaada yake na kazi zake siyo hewa, mfano nchi za Magharibi zinaweza kutoa ahadi ya kuchangia fedha kwenye mfuko wa mabadiliko ya tabianchi lakini kinachoonekana ni kusuasua zaidi.



Makandarasi wa China wakijenga miundombinu Afrika. **PICHA ZOTE: MTANDAO**





# Shule 12 zasajiliwa kupunguza msongamano wa wanafunzi

**Na Jumbe Ismailly,**
MANYONI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida imesajili shule mpya za msingi 12, lengo likiwa ni kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Annastazia Tutuba, alitoa takwimu hizo wakati wa mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Annastazia alikuwa anatoa taarifa za mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha wa 2023/24.

Alizitaja shule zilizosajiliwa ni pamoja Mpandepande, Chimwanzu, Mkambarara, Ihucha, Isinika, Igose, Mbwekoo, Waraka, Checheho, Mpampahu, Mafulungu na Maliki. Aidha, alisema kwa kipindi hicho halmashauri imekarabati shule kongwe mbili za msingi za Kintinku na Makanda kwa kujenga vyumba tisa vya madarasa.

Kuhusu sekta ya kilimo, alisema tani 20 za mbegu ya alizeti pamoja na tani 416 za mbolea ya ruzuku zimesambazwa kwa wakulima 6,713.

Pia, alisema kupitia Idara ya Kilimo wamepokea na kugawa vishikwambi 34 na pikipiki 48 kwa maofisa ugani.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Jumanne Mlagaza, aliwataka maofisa ugani na tarafa kutumia pikipiki walizopewa kwa malengo yaliyokusudiwa ya kuwafikia na kutoa huduma stahiki kwa wananchi.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Kigwe Viziwi, wilayani Bahi, mkoani Dodoma, wakiwa na kompyuta, baada ya kukabidhiwa na shirika lisilo la kiserikali la Kisedeti, shuleni hapo juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa Shule hiyo, Dk. Anderson Ndonu (kulia) na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Sista Mary Sona. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kampeni uhamasishaji nishati safi kupikia yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuunga mkono jitihada za serikali kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, kampuni ya Puma Energy Tanzania kupitia Puma Gas imezindua kampeni iitwayo 'bei kama mkaa faida kibao' yenye lengo la kuhimiza wananchi kupika kwa nishati ya gesi.

Kampeni hiyo imezinduliwa jana mkoani Dar es Salaam, wananchi walielimishwa kuhusu umuhimu wa kutumia nishati safi ya kupikia.

Akizungumza katika kampeni hiyo, Meneja Masoko wa Puma Energy Tanzania, Lilian Kanora, alisema kampeni hiyo inalenga kuelimisha jamii na kuhimiza matumizi ya nishati safi.

Alisema PumaGas inaokoa muda wa mama katika kupika lakini inatoa uhakika kwa mama kutoathirika kiafya kwa kuvuta moshi mwingi akiwa jikoni anapika.

Alisema kupika kwa nishati safi kunasaidia katika ulinzi wa mazingira, kwamba hakutakuwa na sababu ya baba au mama kwenda kukata kuni porini na kuharibu mazingira.

Alisema kampeni hiyo inalenga kumhakikisha mwananchi kutumia fedha kidogo katika kununua nishati safi ukilinganisha na fedha anayotumia kununua mkaa.

"Nitawapa mfano kopo moja la mkaa ni Sh.1,000 hadi Sh.2,000 na kwa familia inayopika milo mitatu kwa siku hii ni sawa na Sh. 2,000 hadi Sh.4,000 kwa siku," alisema na kuongeza:

"Ukipiga hizi hesabu kwa mwezi ni zaidi ya Sh.60,000 wakati PugaGas kilo sita ni Sh.41,000. Katika kampeni hii kutakuwa na punguzo la bei kwa mtungi wa kilo 15 awali mteja alikuwa akipata gesi na mtungi mpya kwa Sh.75,000 ila kwa kipindi hiki kuna punguzo hadi Sh.66,000".

Alisema mtungi wa kilo sita utapatikana kwa Sh.41,000 tu na mtungi wa kilo 38 pamoja na gesi unapatikana kwa Sh.110,000.

Mkuu wa Kitengo cha Mauzo PumaGas, Jeffrey Nasser, aliwataka wananchi wote kuunga mkono kampeni hiyo, huku akishauri hasa wanaume kuwa sehemu ya kuleta mabadiliko kwa kuwezesha familia kutumia nishati safi ya kupikia.

Alisema: "Nitoe rai kwa wanaume ambao ndiyo baba wa familia, kuna msemo wa baba ni kichwa cha familia basi sasa wanaponunua mahitaji ya nyumbani yakiwamo ya chakula wahakikishe wananunua na nishati safi ya kupikia."

# Sekretarieti maadili yawaonya viongozi Mpwapwa

**Na Augusta Njoji,**
MPWAPWA

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imewataka viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kuepuka kukinzana katika utekelezaji wa majukumu yao, ili wananchi wapate huduma bora za kijamii.

Katibu Msaidizi wa Sekretarieti hiyo Kanda ya Kati - Dodoma, Jasmin Awadh alisema hayo jana wilayani humo kwenye mafunzo ya maadili kwa madiwani na wakuu wa idara na vitengo wa halmashauri hiyo.

Alisema viongozi wakikinzana na wasipozingatia uwajibikaji watasababisha ucheleweshwaji wa huduma za kijamii kwa wananchi kama vile hospitali, shule, barabara na wananchi watapoteza imani yao kwa serikali.

Pia, aliwahimiza viongozi hao kushirikiana katika kupanga vipaumbele vya halmashauri ili malengo yaliyopangwa yatekelezwe ipasavyo ikiwamo kuwafikishia wananchi huduma wanazohitaji.

Alieleza kuwa mafunzo hayo ni mkakati na kipaumbele cha sekretarieti hiyo kuhakikisha viongozi wote wanashirikiana katika taasisi zao wanafanya kazi kwa pamoja kwa kuzingatia viwango vya juu vya maadili.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, George Rume, alisema kuwa mafunzo hayo yatawasaidia kuleta mabadiliko katika halmashauri yao na kuzingatia maadili.

Alibainisha kuwa kiongozi yeyote ni lazima ajue dira ya taasisi yake kwamba nini anatakiwa kufanya ili kuwaongoza walio chini yake kuitekeleza na kuleta maendeleo kwa wananchi na serikali kwa ujumla.

# Vituo 60 vya upasuaji wajawazito kujengwa Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Myeka Simon amesema uongozi wa mkoa huo umepanga kuwa na vituo 60 vinavyotoa huduma za dharura za upasuaji kwa wajawazito wenye vidokezo vya hatari.

Alisema hayo jana wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa huduma za afya ya uzazi na mtoto unaofadhiliwa na Shirika la (KOFIH) la nchini Korea.

Mradi huo utatekelzwa kwa kipindi cha miaka mitano katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa na Mpwapwa.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, alisema kuwa Mkoa wa Dodoma una vituo vya afya 546, hospitali 17, vituo vya afya 68, zahanati 431 na kliniki 30.

Alisema pia una vituo 416 vinatoa huduma za afya ya uzazi na mtoto na vituo 48 sawa na asilimia 56 kati ya vituo 85 vinatoa huduma za dharura za upasuaji kwa wajawazito.

Alisema kuwa vituo 44 vipo ngazi ya msingi (vituo vya afya, hospitali za halmashauri) hilo ni ongezeko kubwa kwani mwaka 2020 kulikuwa na vituo 29 vinavyotoa huduma ya upasuaji ukilinganisha na vituo 48 mwaka 2024.

Aidha, alisema taarifa ya utafiti uliofanyika mwaka 2020 ya viashiria vya huduma za afya ya uzazi Mkoa wa Dodoma umefanya vizuri kulinganisha na takwimu za kitaifa.

Alisema, baadhi ya matokeo ya viashiria hivyo ni kinamama waliojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya kitaifa ilikuwa ni asilimia 81 na kwa Mkoa wa Dodoma ilikuwa ni asilimia 90.0.

Myeka alisema kinamama waliozalishwa na watoa huduma wenye ujuzi kitaifa ilikuwa asilimia 84.8 na kwa Mkoa wa Dodoma ilikuwa asilimia 93.2.

Aidha, alisema wajawazito waliohudhuria kliniki mahudhurio manne au zaidi kitaifa ilikuwa asilimia 65 na kwa Mkoa wa Dodoma ilikuwa asilimia 76.8.

Alisema mradi huo unatekelezwa kwa miaka mitano, ulianza mwaka 2021 na unatarajia kumalizika mwaka 2025.

Alisema, katika kipindi cha miaka mitatu 2021-2023 ya utekelezaji wa mradi Sh. bilioni 2.7 zimetumika katika kutekeleza shughuli mbalimbali.

Ofisa Programu wa Uzazi Salama, Idara ya Afya ya Uzazi Mama na Mtoto Wizara ya Afya, Fideo Obimbo, alisema: "Mradi huu unakwenda sambamba na jitihada za serikali kupunguza vifo vya mama na mtoto, ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu.



# RC aagiza 'vikoba' vya walimu kuchunguzwa

Na Nebart Msokwa,
MBEYA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC) imetakiwa kufuatilia taratibu za uendeshaji wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) za walimu kwa maelezo kuwa zimekuwa zikikabiliwa na matatizo mbalimbali.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa agizo hilo wakati wa uzinduzi wa taarifa ya utendaji wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo kwa mwaka wa 2023, uliofanyika jijini Mbeya.

Homera aliomba viongozi wa TCDC kusimamia kwa ukaribu vyama vya ushirika vya walimu ili kubaini chanzo cha kuwapo kwa migogoro ya mara kwa mara pamoja na kuchukua hatua za haraka kutatua migogoro hiyo ambayo imekuwa ikichangia kupoteza raslimali.

"Pamoja na mafanikio makubwa ya vyama hivi nchini lakini niombe viongozi wa tume tuziangalie tena SACCOS za walimu zimekuwa na migogoro mingi, siyo hapa Mbeya tu hata mikoa mingine niliyohudumu nimeona tatizo hili," alisema Homera.

Alivitaka vyama hivyo kutoa elimu kwa wanachama ili watoke kwenye mikopo umiza na kuingia kwenye SACCOS, sambamba na kupunguza masharti ya mikopo huku akisisitiza watendaji kuwa waaminifu kwa kulinda rasilimali za wanachama ili wapate stahiki zao.

**"Pamoja na mafanikio makubwa ya vyama hivi nchini lakini niombe viongozi wa tume tuziangalie tena SACCOS za walimu zimekuwa na migogoro mingi, siyo hapa Mbeya tu hata ...**

Akiwasilisha taarifa ya utendaji wa SACCOS kwa mwaka 2023, Mrajis wa vyama vya ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dk. Benson Ndiege, alisema lengo la kuzindua taarifa hiyo ni kuweka uwazi wa taarifa ya utendaji wa vyama hivyo nchini.

Vilevile, alisema wanalenga kujadili fursa na changamoto za sekta hiyo pamoja na kuonesha mchango wa sekta kwenye pato la taifa na fursa za ajira zilizoko kwenye sekta hiyo.

Alisema kwa mwaka 2023, jumla ya SACCOS 884 zimepewa leseni ya kuendesha biashara ya huduma ndogo za fedha nchini, huku nyingine 331 zikikosa leseni kutokana na kutokidhi vigezo.

Aidha, alisema idadi ya wanachama wanaonufaika na huduma hizo imeongezeka kutoka milioni 1.80 mwaka 2022 hadi milioni 1.82 ambapo pia mitaji ya SACCOS imeongezeka kutoka Sh. bilioni 151.05 hadi kufikia Sh. bilioni 180.40.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo (Ushirika na Umwagiliaji), Dk. Suleiman Serera, alizitaka SACCOS kutoa takwimu halisi kwenye utendaji wao na kuahidi wizara kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha sekta hiyo inaendelea kuimaraika na kukua zaidi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, wilayani Chunya, mkoani Mbeya, Tamim Kambona (kushoto), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi wa Kampuni ya AMJ Global Mult Contractors Ltd, Adam Sikigoye, baada ya kutiliana saini mkataba wa ujenzi wa kituo cha mabasi cha halmashauri hiyo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wananchi wawasilisha kilio ubovu barabara kwa mbunge

Na Elizabeth John,
NJOMBE

WAKAZI wa Kata ya Kitandililo Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe wameomba kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara na umeme katika maeneo yao, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii.

Walitoa wito huo juzi katika mkutano wa Mbunge wa Makambako, Deo Sanga uliofanyika katika vijiji vya Kitandililo, Nyamande na Ibatu.

Mmoja wa wananchi hao akiwamo, Moses Msigwa alisema bado kuna changamoto ya barabara kutopitika pamoja na kukosekana kwa umeme kwenye baadhi ya vitongoji.

Elia Mpalate aliwaomba Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini kuboresha miundombimu ya barabara pamoja na Daraja la Nyamande Mahongole ambalo limekua adha kubwa kwao.

Naye Nicolaus Mlonganile alisema tatizo la umeme ni kubwa na hivyo wamekuwa wakilalamika mara kwa mara bila ya mafanikio.

"Kwetu sisi tunaona umeme ni anasa kwa sababu tumekuwa tunalia muda mrefu na miaka mingi ni kweli kwenye vijiji umekuja lakini kwenye vitongoji haujafika tutaandikishwa majina hadi lini? alihoji Mlonganile.

Ofisa kutoka Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Njombe, Eliasi Mwaituka, alisema barabara hizo zitaendelea kuboreshwa kwa kadri fedha zinavyopatikana. Mwakilishi wa Meneja wa TANESCO Makambako, Zaidat Ngoda, aliwataka wananchi wanaokosa umeme kufikisha taarifa ya kimaandishi ili kuombea miradi pamoja na kuwataka wananchi kulinda miundombinu.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Nakembweta Makala, alisema kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 halmashauri imekusudia kuboresha huduma za kijamii hasa katika sekta ya afya na elimu.

Mbunge wa Makambako, Deo Sanga alisema katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 Halmashauri ya Makambako imetengewa bajeti ya Sh. bilioni 33.6 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Pia aliahidi kuchangia saruji mifuko 130 ili itumike katika ujenzi wa nyumba za walimu Kata ya Kindililo na bati 70 kwa ajili ya kupanua nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Nyamande.

# Bil.3/- kujenga kituo cha mabasi Chunya

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya imeanza kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kujenga kituo cha kisasa cha mabasi.

Hatua hiyo ni baada ya kusaini mkataba wa zaidi ya Sh. bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

Agosti 6, 2022 Rais Samia akiwa ziarani wilayani Chunya aliagiza halmashauri hiyo kutumia mapato ya ndani kujenga kituo cha mabasi baada ya wananchi kulalamika kukosa kituo hicho.

Mkataba wa ujenzi wa kituo hicho ulisainiwa juzi, kati ya halmashauri hiyo na kampuni ya Malk Consultants LTD ambapo unatarajiwa kuanza kutekelezwa Septemba 16 mwaka huu na kukamilika Juni 15, 2025.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chunya, Tamimu Kambona, alisema mradi huo utakuwa na miundombinu mbalimbali ikiwapo vibanda 400 vya biashara na eneo la maegesho lenye uwezo wa kuchukua mabasi 100 kwa wakati mmoja.

Alisema lengo la ujenzi wa kituo cha mabasi ni kuboresha huduma ya usafiri ili kuondoa adha kwa wananchi ambao walipaza sauti kwa Rais Samia Suluhu Hassan alipokuwa ziarani wilayani humo.

"Tunatekeleza kwa njia ya kandarasi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya Mwaka 2023 ambapo mradi ulitangazwa kupitia mfumo wa NeST kumpata mkandarasi mwenye sifa kulingana na taratibu za manunuzi," alisema Kambona.

Katika hafla hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa maelekezo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani humo kushirikiana na halmashauri kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha huduma za usafiri zinaboreshwa ili kuchochea shughuli za kiuchumi na kuonya kusiwapo kwa ubadhirifu wa fedha za mradi huo.

"TAKUKURU ina imani na ninyi muda uliopo kwenye mkataba wa mradi huo ukamilike, pia niombe machifu kushirikiana na serikali kuhakikisha unakuwa na tija na kunufaisha wananchi," alisema Homera.

Alisema atahakikisha anatembelea mara kwa mara mradi huo, ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati uliopangwa na thamani halisi ya fedha zilizotengwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri, Bosco Mwanginde, alisema ujio wa mradi huo utakuwa suluhisho kwa wananchi hususani kwa wafanyabiashara kwa maelezo kuwa kutajengwa vibanda 400 kwa ajili ya shughuli za biashara kutapunguza tatizo la uhaba wa masoko.

Alisema: "Wananchi wanakwenda kuongeza wigo mpaka wa shughuli za kiuchumi na ndiyo maana mradi huu unatekelezwa kwa mapato ya ndani ya halmshauri ikiwa ni miongoni mwa miradi ya kimkakati".

Hivyo, aliwataka wananchi kushirikiana na halmashauri hiyo kwenye utekelezaji wa mradi huo ikiwa ni pamoja na kushiriki kwenye shughuli za ujenzi hasa vijana.

# Wizara ya Ujenzi kuendana na mageuzi ya kidunia

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema imejipanga kuendana na mageuzi ya kidunia inayoendana na sekta ya ujenzi.

Hivyo, imeanza kufanya mapitio ya sera na sheria kwa kushajihisha usajili wa wahandisi na kampuni za ujenz ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Habiba Hassan Omar wakati akifunga Kongamano la Miaka 50 la Chuo Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Karume (KITS) Zanzibar.

Alisema hatua hiyo itaimarisha usimamizi wa utoaji wa huduma bora na kupatikana ujenzi bora na salama.

Hivyo, aliwataka wahandisi kujijenga kimadili kwa kuheshimu taaluma zao na kuepukana na matendo na tabia zinazokwenda kinyume na maadili ya kazi zao.

Aidha aliwataka kuepuka na vitendo vya rushwa, kuitia hasara serikali na wateja wao kwa kuwa na usanifu, ukadiriaji na usimamizi bora wenye viwango vinavyohitajika na gharama zinazostahiki.

Pia alitaka kufanyike ushajihishaji wa watoto shuleni hasa watoto wa kike kupenda kusoma masomo ya sayansi ili kujiunga na masomo ya juu katika fani mbalimbali za uhandisi.

Dk. Habiba alisema kwa mujibu wa takwimu Zanzibar kuna wahandisi 361, kati yao wanawake ni 75, hivyo bado kuna safari ndefu za kuleta uwiano wa kijinsia katika fani ya uhandisi na teknolojia.

Mmoja wa washiriki hao, Fatma Kara, alisema uhandisi ni fani muhimu, kwamba kukua kwa sekta ya utalii kumefungua fursa nyingi ikiwemo ya ujenzi wa majengo ya hoteli za kitalii.

Alisema ni muhimu fani hiyo ikisomewa na jinsia zote na KITS kiendelezwe zaidi ili sekta ya ujenzi isaidie maendeleo ya nchi.

Fatma alisema Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Salmin Amour Juma ndiye aliefungua milango ya wahandisi wanawake Zanzibar kutambulika, kwamba yeye ni miongoni mwa wanufaika hao.

Alisema katika uongozi wa Rais huyo kulijengwa jengo la Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) eneo la Kinazini ambalo sasa linatumika kwa ofisi za Umoja wa Mataifa (UN).

# Ataka wakufunzi wapewe nyenzo kuendana na teknolojia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mafunzo ya Amali, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Bakari Ali, amesema kuna haja kuongeza kasi ya kutoa mafunzo kwa walimu, ili kukabiliana na maendeleo ya teknolojia yanayokuwa kwa kasi nchini.

Aliyasema hayo jana Zanzibar, wakati akifungua mafunzo kwa walimu na wakufunzi 82 wa vyuo vya kati vitatu vilivyopo Unguja.

Alisema Tanzania ya viwanda inategemea zaidi wahitimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali watakaozalishwa na wakufunzi mahiri.

Alisema Serikali ya Muungano na Zanzibar zinaelekeza taasisi za elimu kuwapatia vijana ujuzi utakaowawezesha kujiajiri baada ya kumaliza mafunzo yao.

Alisema kwa kulitambua hilo serikali imefanya mageuzi makubwa katika elimu ya msingi na sekondari na kusisitiza lazima kuwepo mitaala na walimu wanaozingatia umahiri wakati wa kufundisha, ili kuzalisha wataalam waliobobea.

Hivyo, aliwasisitiza viongozi wa vyuo hivyo wanaporatibu mafunzo kama hayo kuzingatia maadili mema ili kuzalisha wataalamu wa baadaye watakaofanya kazi kwa uaminifu na weledi.

Bakari alisema sifa za mfanyakazi imara ni uaminifu, uadilifu na umahiri na ndiyo nguzo muhimu katika elimu na taasisi zote za ufundi.

Hata hivyo alisema kwa Zanzibar Mamlaka ya Mafunzo ya Amali inatoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wakufunzi wa mafunzo ya amali kwa kutumia mfumo wa mtaala mahiri.

Ofisa Udhibiti Ubora wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTIVET), Muhammed Abdallah Mbasha, alisema ni matarajio yake kuwa walimu watapata umahiri katika kuchambua na kufundisha mitaala hiyo .

Mkurugenzi wa Chuo cha Microtech, Said Saleh alisema ni muhimu kuwa na umoja wa vyuo vya kati Zanzibar na mafunzo hayo yawawezesha walimu kufanya kazi zao kwa umahiri katika kutoa elimu kwa wanafunzi.

Mkuu wa Chuo cha Afya cha Imperial, Jokha Khamis Juma alisema ushirikiano huo ni muhimu kwa kunyanyua umahiri wa walimu.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma (wa tano kushoto waliosimama), Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Anna Athannas Paul (wa nne kushoto waliosimama), wakizungumza na wajasiriamali wa Chuo cha Wajasirimali Wanawake cha Bare Foot College cha Kinyasini Mkoa wa Kaskazini Unguja, walipowatembelea juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wakumbushwa kulipa kodi kwa hiari

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Said Ali Mohamed amewataka walipa kodi kutimiza wajibu wao, ili serikali itoe huduma bora kwa wananchi.

Aliyasema hayo kwa nyakati tofauti alipokuwa akikamilisha ziara ya kuwatembelea na kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili wamiliki wa hoteli katika Mkoa wa Kaskazini na Kusini Unguja.

Aidha, aliwahakikishia walipakodi hao kuwa changamoto walizozitoa amezipokea na wapo tayari kuzifanyia kazi kwa lengo la kuimarisha huduma bora kwa walipakodi hao.

Alisema ZRA haitasita kuwachukulia hatua wale wote watakaokikuka sheria kuikosesha serikali mapato ambayo ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo ya sekta mbalimbali kisiwani humo.

Meneja wa Hoteli ya Essque Zalu Zanzibar, Fatma Al Sinawi, alipongeza uamuzi wa ZRA kuwatembelea na kutumia mifumo ya kidijitali inayowarahisishia kulipa kodi kwa urahisi zaidi.

Mdhibiti wa Fedha wa Hoteli ya The Residence, Jimmy Mbute, alisema wataendelea kuwa walipakodi wazuri kwa maendeleo ya Zanzibar.

# Watakiwa kutunza vifaa vya uchukuaji taarifa baharini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAVUVI wamekumbushwa kuvitunza vifaa vya uchukuaji wa taarifa baharini ili ziwasaidie katika majukumu yao ya kukusanya taarifa

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Soud Hamed, wakati wa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wavuvi yaliyolenga matumizi ya vifaa vya kisasa vitavyofungwa katika vyombo vya wavuvi baharini.

Alisema ufungwaji wa vifaa hivyo katika boti za uvuvi kutasaidia kuona taarifa za uvuvi juu ya gharama zitazitumika na kujua kina cha joto katika maeneo yatayotumika kwa shughuli za uvuvi.

Aidha, aliwataka wavuvi kuvitumia vifaa hivyo kupata taarifa za kutatua changamoto zao ili kila mmoja wao afurahie neema za uchumi wa bluu kwa kuwawezesha wavuvi na watumiaji wengine wa baharini.

Sambamba na hayo alisema hakutakuwa na mkataba wowote kwenye ufungaji wa vifaa hivyo, huku akiwataka wavuvi hao kuvitunza na kuvitumia ipasavyo kwa kufuata miongozo ya iliyotolewa ili kufikia malengo ya serikali ya kuwasaidia wavuvi wadogo.

Mtafiti wa Ikolojia ya Samaki, Hellen Joseph Kizenga, kutoka Taasisi za Bahari katika Chuo Kikuu cha Dar es Salam (UDSM) alisema lengo la kukutana na wavuvi ni kuona namna gani ya kusaidia kutoa taarifa za utafiti wa bahari kwa kuwa wao ndiyo watumiaji wakuu wa rasilimali hizo.

Ofisa TEHAMA kutoka Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Nassor, Abdalla Nassor aliwataka wavuvi kushirikiana na wataalamu juu ya utumiaji wa vifaa hivyo, ili kukuza uvuvi wa kisasa kwa maslahi ya sasa na kizazi cha baadae

Mwenyekiti wa wavuvi wadogo, Omar Mohd Ali, aliziomba taasisi husika kuwaekea mfumo wa huduma za msaada kwa wavuvi wakati wa kufikwa na maafa baharini

Utoaji wa vifaa hivyo ni utekelezaji wa mradi wa pamoja kati ya Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Bahari, Taasisi ya Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salam na Taasisi ya WIOMSA.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**STEPHEN SAID MMBAJI** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 772 CEQ. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MOR/KIL/30309/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**KAGOLI L. PETER** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index **No. S4968-0022** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. **FRANCIS DE SALES MISSION SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018, Cheti hiki kimepotea Mkoani TABORA. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: TAB/RB/4034/202**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ROBERT ANYOSISYE MWANKEJELA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0434-0107 kilichotolewa na Ndembela Secondary Mwaka 2006. Cheti cha chuo chenye namba No.00565 kilichotolewa na Tanzania Public Service College (TPSC) mwaka 2009. cheti cha chuo chenye namba 003575 kilichotolewa na Tanzania Institute of Accountancy (TIA) mwaka 2013. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/192535/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RICHARD HENRY ISINIKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 914 DMW** yenye jina la Bugumba Peter Kapaya. Kwa yeyote atakaeye iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **PHQ/SHI/KAH/7514/2024.**

## KIWANJA KINAUZWA

KIWANJA CHENYE UKUBWA WA **SQM1698** CHA KUJENGA HOTEL KINAUZWA MEDELI WEST DODOMA MJINI JIRANI MORENA HOTEL NYUMA YA SHOPPERZ BEI **TSH 185, 000,000** KINA HATI MILIKI. KWA MAWASILIANO ZAIDI **PIGA SIMU NAMBA : 0655660730**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ADOLF ALFREDUS KATAMBI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC533CXH** aina ya Dayun **DY 200.** Chassis **No. L7GPCMLD6M1023023.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/39511/2024**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya Rungwe**
**Kituo cha MASEBE Mkoa wa Mbeya**
**Shauri la Ndoa No. 4/2024**
**Jina la mdai: ISAKA MWASEGE**
**Jina la mdaiwa: AMINA V. KAJINGA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa: AMINA V. KAJINGA**
**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**

**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 24 Mwezi wa 9 Mwaka 2024 saa 3 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 3 Mwezi wa 9 Mwaka 2024.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai Na. 111/2024**
**JINA LA MDAI ...........JOSEPHINE BONIFACE NDAGA**
**JINA LA MDAIWA ......NOVATUS MICHAEL KALIATA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya ni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA**
**NOVATUS MICHAEL KALIATA**
**0718 812 552**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO**

Kwa hiyo unatakiwakuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 19 mwezi 09 mwaka2024saa 2:30 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajil iya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi 09 Mwaka 2024.

## KUPOTEA KWA CHETI



**MICHAEL NIKOLAUS REUBEN** anatangaza kupotea kwa cheti cha Chuo chenye **No. AEA/D/2015/0190** Kilichotelewa na **CHUO KUKUU CHA KILIMO SOKOINE** mwaka 2018 pomoja na cheti cha matokeo(Transcript) cheti hiki kilipotea Mkonze- Dodoma. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/DOD/38507/2024**

## TANGAZO, TANGAZO MNADA WA NYUMBA

**FAGIO BROKERS** kwa idhini tuliyopewa na **SAJFA MICROFINANCE CO. LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba moja mali ya **SAMWELI NDILE** iliyopo Kitongoji cha Mji Mwema – Mlowo.

Mnada utafanyika siku ya Ijumaa tarehe 13/09/2024 kuanzia saa 5:00 kamili asubuhi eneo nyumba ilipo.

**MASHARTI YA MNADA**

- Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei ya nyumba na salio la 75% limaliziwe ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya mnada.
- Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi.

**MAWASILIANO: 0786606041/0768224862/0758063383.**

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@ GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WAKULIMA TEA CO LIMITED** anatangaza Kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TATA MODELSD1015** yenye usajili namba **T362BRX CHASSIS NAMBA: MAT420203A2R28288** na **ENGINE NAMBA: B591452001L62956188.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/MBE/RUN/27705/2024**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 303 LA 2023**
**BRUNO THOBIAS**
**BRUNO.........MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**HAMIDU ABDALLAH............MDAIWA/WADAIWA**

**WITOKUITWA SHAURINI**

**HAMIDU ABDALLAH**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**BRUNO THOBIAS BRUNO** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa /kusikilizwa tarehe 30/9/2024 saa TATU Asubuhi mbele ya Mh. J.W SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 10 mwezi 09, 2024

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Shambulio la Israel laua 40 Gaza

**GAZA,** Palestina

MAMLAKA ya ulinzi wa raia inayosimamiwa na Hamas katika Ukanda wa Gaza imesema takriban watu 40 wameuawa na wengine kadhaa kujeruhiwa baada ya Israel kufanya shambulizi kwenye eneo la kibinadamu.

Kwa mujibu wa mamlaka hiyo, shambulio hilo lilitekelezwa katika eneo la kibinadamu huko Khan Younes usiku wa kuamkia jana, huku Israel ikisema imelenga kitovu cha operesheni cha Hamas.

Ofisa wa ulinzi wa raia wa Gaza, Mohammed Al-Mughai, alisema katika shambulio hilo pia watu 60 wamepatikana na majeraha na kuhamishiwa katika hospitali za karibu.

"Timu zetu bado zinafanya kazi kutafuta watu 15 ambao hawajulikani waliko baada ya shambulio ambalo limelenga mahema ya watu waliokimbia makazi yao huko al-Mawasi, Khan Younes mji ulio kusini mwa Ukanda wa Gaza," alisema.

Shirika linalohusika na huduma za dharura katika Ukanda wa Gaza, lilisema mashimo makubwa yamesababishwa na shambulio la Israel.

"Familia zote zilitoweka katika mauaji ya Al-Mawasi huko Khan Younes, chini ya mchanga, kwenye shimo refu," msemaji mwingine wa ulinzi wa raia, Mahmoud Basal amesema katika taarifa.

Jeshi la Israel lilieleza kuwa limelenga eneo hilo baada ya kubaini kuwapo kwa makada wa Hamas katika eneo hilo.

"Ndege ya Jeshi la Israel imewashambulia magaidi wakuu wa Hamas waliokuwa wakiendesha shughuli zao katika kitovu cha operesheni na udhibiti ndani ya eneo la kibinadamu la Khan Younis," jeshi lilisema.

"Makundi ya kigaidi katika Ukanda wa Gaza yanaendelea kutumia vibaya miundombinu ya kiraia na ya kibinadamu, ikiwa ni pamoja na eneo lililoteuliwa la kibinadamu, kutekeleza shughuli za kigaidi dhidi ya Israel na askari wa IDF," jeshi lilisema.

Wakati huo huo, Hamas ilikanusha kuwa na wapiganaji katika maeneo ya kibinadamu.

Al-Mawasi, katika mji wa Khan Yunis, iliteuliwa kuwa eneo salama na jeshi la Israel mwanzoni mwa vita, na maelfu ya Wapalestina waliokimbia makazi yao walipata hifadhi katika eneo hilo.

Hata hivyo, Jeshi la Israel liliendelea kufanya operesheni mara kwa mara katika eneo hilo, ikiwa ni pamoja na shambulio la Julai, mwaka huu, ambalo mamlaka ya afya ilisema iliua zaidi ya watu 90, ikiwa ni pamoja na kiongozi wa kijeshi wa Hamas Mohammed Deif.

Ili kuhalalisha mashambulizi hayo, Israel inaeleza kuwa Hamas mara kwa mara huwatumia raia kama ngao za binadamu, jambo ambalo kundi hilo linakanusha. **RFI**

# EU, Marekani watishia kuwaadhibu Iran

**TEHRAN,** Iran

MAREKANI na Umoja wa Ulaya (EU) wamesema wamepokea taarifa za kuaminika za kiintelejensia kutoka kwa washirika wake zinazoonesha kwamba Iran imeipatia Russia makombora ya masafa, wakisisitiza kwamba watajibu endapo taarifa hizo zitathibitishwa.

Hayo yalielezwa jana na msemaji wa EU, Peter Stano, akieleza kuwa wanazo habari juu ya taarifa za kuaminika zilizotolewa na washirika wao za kupelekwa kwa makombora ya masafa marefu ya Iran nchini Russia.

Alisema viongozi mjini Brussels wanazifuatilia kwa karibu taarifa hizo na iwapo itathibitika umoja huo utachukua hatua kali na za pamoja za kuiadhibu Iran.

Washington nayo imetoa matamshi sawa na hayo ikisema imejiandaa kuchukua hatua zitakazoiathiri Iran.

Vyombo kadhaa vya habari vya Marekani viliripoti wiki iliyopita kwamba Washington inaamini Iran imeipelekea Russia silaha za kutumia kwenye vita dhidi ya Ukraine.

Maofisa wa EU na Marekani wamesema ikiwa taarifa hizo ni sahihi itakuwa ni kutanuka pakubwa kwa msaada wa Tehran kuelekea Russia katika uvamizi wake wa kijeshi nchini Ukraine.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Iran, Nasser Kanani, alikanusha vikali madai hayo, huku Russia ikijizuia kutoa jibu la moja kwa moja.

"Tunakanusha vikali madai ya kuihusisha Iran na upelekaji silaha upande mmoja wa vita," alisema Kanani.

Kwa upande wa Russia haikutoa tamko lolote la kukanusha madai hayo hata pale msemaji wa Ikulu ya Kremlin, Dmitry Peskov, alipoulizwa moja kwa moja juu ya ripoti za jarida la Wall Street kwamba Iran imeipatia Moscow makombora.

"Tumeiona hiyo ripoti, siyo kila wakati aina hii ya taarifa huwa za kweli. Iran ni mshirika wetu muhimu, tunaimarisha mahusiano yetu ya kibiashara na kiuchumi, tunatanua ushirikiano wetu na mashauriano kwenye maeneo yote yanayowezekana, ikiwamo yale yaliyo nyeti kabisa," alisema Peskov.

Wakati huo huo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Ukraine, iliandika kupitia mtandao wa Telegram kwamba imemwita mkuu wa kituo cha uwakilishi wa ubalozi wa Iran Shahriar Amouzegar kumtahadhirisha kwa matamshi makali juu ya athari katika mahusiano ya mataifa hayo iwapo habari hizo zitathibitika.

Kwa miezi kadhaa sasa mataifa ya magharibi yamekuwa yakiionya Iran dhidi ya kupeleka makombora nchini Russia, na kwamba EU tayari ulikwisha iadhibu nchi hiyo kwa vikwazo kutokana na uamuzi wake wa kuipatia Moscow ndege zisizo na rubani kuzitumia katika vita vya Ukraine.

"Tumeweka bayana kabisa kwamba tumejitayarisha kutoa adhabu inayostahili endapo taarifa hizo zitathibitika," alisema Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Marekani Vedant Patel.

**DW**



Wananchi nchini Pakistan wakiwa wamekusanyika kushinikiza kuachiwa kwa mmoja wa viongozi wakuu wa chama cha waziri mkuu wa zamani, Imran Khan, aliyewekwa kizuizini hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

## Tani 2.63 za cocaine zanaswa Guinea

**BISSAU,** Guinea

POLISI nchini Guinea-Bissau wamesema wamekamata tani 2.63 (kilo 2,630) za cocaine iliyopatikana kwenye ndege iliyowasili kutoka Venezuela katika mji mkuu wa nchi hiyo ya Afrika Magharibi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na maofisa usalama hao, walinasa marobota 78 ya dawa hizo ambazo ziliingizwa kinyemela kwenye ndege ya Gulfstream IV wakati wa uvamizi Jumamosi alasiri kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Osvaldo Vieira wa Bissau.

Ilielezwa kuwa wafanyakazi watano wa ndege hiyo, akiwamo rubani, walikamatwa, pamoja na raia wawili wa Mexico, Colombia, Ecuador na Brazil.

Taarifa ya polisi ilisema washukiwa hao watafikishwa mbele ya mahakama ya mkoa kwa mahojiano, na hatua zingine kwa mujibu wa sheria za nchi hiyo.

Polisi walisema uvamizi huo ulifanywa kwa ushirikiano na Utawala wa Utekelezaji wa Dawa za Marekani, Kituo cha Uchambuzi na Operesheni za Bahari-Narcotics.

Ilielezwa kuwa wasafirishaji wa dawa za kulevya mara nyingi hutumia nchi za Afrika Magharibi kama njia ya kusafirisha kokeini kutoka Amerika Kusini hadi Ulaya.

Kwa mujibu wa ripoti ya Umoja wa Mataifa ya Dawa za Kulevya ya 2024, Cocaine imesalia kuwa miongoni mwa dawa zinazotumika sana duniani kote ikiwa na watumiaji milioni 23. **TRT**

# MAREKANI YAONGEZA WIGO KWA VIJANA MICHUANO NDONDO CUP

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MICHUANO ya Ndondo Cup 2024, inaendelea jijini Dodoma baada ya kuanza mwishoni mwa wiki, huku ikiangazia dhamira thabiti ya Serikali ya Marekani ya kuunganisha michezo na mipango muhimu ya afya inayolenga kupambana na VVU na kukuza chanjo miongoni mwa vijana wa Tanzania.

Katika mpango huo ambao unaongozwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) na Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Ukimwi (PEPFAR) kupitia mradi wa Breakthrough ACTION, unaifanya michuano hiyo ya soka ya ngazi ya chini kuvuka mipaka ya matukio ya jadi ya michezo, yakitumika kama jukwaa lenye nguvu la elimu ya afya na ushirikishwaji wa jamii.

Kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana kutoka kwa matukio ya awali ya Ndondo Cup yaliyofanyika Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Mwanza na Ruvuma - ambapo makumi ya maelfu walipata huduma muhimu za afya - mashindano ya mwaka huu yanalenga kuongeza ushawishi wake kupitia kampeni ya vijana ya 'Sitetereki' na mpango wa chanjo wa 'Kuwa Bingwa'.


Mwakilishi wa USAID, Moses Bateganya, alisisitiza ushirikiano kati ya michezo na afya kwa kueleza: "Tumejizatiti kuanzisha mbinu za ubunifu zinazotoa matokeo halisi ya afya. Tunaamini michezo inaweza kuwa nguvu kubwa katika kuleta na kukuza mabadiliko chanya ya tabia na kuboresha upatikanaji wa huduma, na tunafurahi kushirikiana na Ndondo Cup na Serikali ya Tanzania kuleta mpango huu katika uhalisia."

Evangelina Chihoma kutoka Mfuko wa PEPFAR, yeye alisisitiza umuhimu wa kuwafikia vijana, akiangazia takwimu za utafiti uliofanyika hivi karibuni ukionesha kuna haja kubwa ya kufikia vijana na elimu ya huduma za VVU.

"Mfuko wa PEPFAR unaendelea kujizatiti kupambana na VVU Tanzania" alisema. "Lengo letu ni kufikia vijana kwa njia mablimbali za kibunifu kama Kombe la Ndondo".

Kampeni ya 'Sitetereki' inalenga hasa vijana wenye umri wa miaka 15-24, ikiwawezesha kuchukua jukumu la afya zao. Washiriki wanaweza kupata taarifa muhimu kuhusu VVU, kupima, kupata kinga kabla ya maambukizi (PrEP), tiba ya kufubaza virusi vya ukimwi yaani antiretroviral (ART), iwapo wamepimwa na kupatikana na VVU, yote haya wakifurahia msisimuko wa michuano hiyo.

Wakati huo huo, mpango wa 'Kuwa Bingwa' unahimiza wanaume kuweka kipaumbele kwenye chanjo, huku huduma za chanjo zikifikika kwa urahisi kwenye uwanja wa michezo, zikiimarisha umuhimu wa afya kwao na familia zao.




Mwakilishi wa USAID, Moses Bateganya (wa pili kushoto), akikabidhi zawadi ya mchezaji bora wa mechi ya ufunguzi wa mashindano ya Ndondo Cup Dodoma kwa mchezaji wa Nkuhungu Terminal FC, Kassim Hussein, baada ya mechi dhidi ya Kikuyu FC iliyopigwa jijini humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtibwa Sugar kuanza safari ya Ligi Kuu Sept. 20

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mtibwa Sugar iliyoshuka daraja msimu uliopita, itaanza kampeni yake ya kutaka kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara nyumbani, Septemba 20, mwaka huu, katika Uwanja wa Manungu uliopo Turiani, Morogoro, itakapowavaa Maafande wa Green Warriors katika mchezo huo wa ufunguzi wa Ligi ya Championship.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), inayoonesha kuanza kwa ligi hiyo, Septemba 20, timu nyingine iliyoteremka daraja msimu huu, Geita Gold nayo itakuwa nyumbani Septemba 21 katika Uwanja wa Nyankumbu, Geita kukipiga na TMA.

Katika ratiba hiyo inaonesha kuwa kutakuwa na mechi mbili za ufunguzi, ambapo mbali na Mtibwa dhidi ya Green Warriors, mechi nyingine siku hiyo itakuwa ni kati ya Mbeya City itakayocheza uwanja wake wa nyumbani, Sokoine Mbeya, dhidi ya Bigman FC, ambayo zamani ilijulikana kwa jina la Mwadui FC.

Septemba 21 pia kutakuwa na michezo mitatu, ambapo mbali na Geita Gold dhidi ya TMA, pia kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani, Cosmopolitan itaialika African Sports, ambapo Songea United itakuwa nyumbani, Uwanja wa Majimaji kuvaana na Mbeya Kwanza.

Mechi zingine tatu za kumalizia raundi ya kwanza zinatarajiwa kupigwa Septemba 22, pale Polisi Tanzania itakapocheza dhidi ya Mbuni kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi, huku Biashara United ikiwa Uwanja wa Karume, Musoma, Mara dhidi ya Transit Camp, wakati Kiluvya FC yenyewe itashuka Dimba la Mabatini, Mlandizi kupepetana na Stand United.

Ratiba inaonesha kuwa raundi ya pili itapigwa Septemba 27, wakati Stand United itakapoikaribisha Transit Camp, Uwanja wa Kambarage, Shinyanga, Cosmopolitan dhidi ya Mtibwa Sugar Uwanja wa Mabatini, Mbeya City dhidi ya Mbeya Kwanza katika dimba la Sokoine.

Septemba 28, mwaka huu, Green Warriors itakipiga dhidi ya African Sports, Mabatini, Polisi Tanzania dhidi ya TMA Uwanja wa Ushirika, Biashara United dhidi ya Kiluvya, Karume, na Septemba 29, raundi itahitimishwa kwa mchezo kati ya Songea United dhidi ya Bigman FC.

## Mafunzo yajisifu kuvuna alama tatu kwa KMKM

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

KLABU ya Mafunzo, imesema alama tatu walizozipata katika mchezo wao walioita ‚mgumu' wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya KMKM SC zimewapa furaha hasa kwa kuona kiwango kizuri cha wachezaji wao.

Maafande hao wa Mafunzo SC waliwafundisha soka maafande wenzao wa KMKM SC kwa kuwafunga bao 1-0 katika mwendelezo wa Ligi Kuu ya Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), kwenye mchezo uliochezwa juzi katika viwanja vya nje vya New Amaan Complex.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Kocha Msaidizi wa Mafunzo SC, Abdallah Bakari, alisema kupata ushindi katika mchezo wa kwanza wa ligi kunatia matumaini si tu kwa wachezaji, lakini pia hata kwa benchi lao la ufundi.

Alisema wamecheza mchezo mgumu dhidi ya KMKM ambapo kila timu inajua uwezo wa wapinzani wao.

Bakari alisema ushindi huo haukutokana na bahati, kwani ni jitihada kubwa za wachezaji kuhakikisha hawafanyi makosa hasa katika mchezo huu wa kwanza.

"Huu si ushindi wa bahati, bali ni ushindi ambao wachezaji walijituma ili kuona nini tunafanya katika mchezo huu wa kwanza,“ alisema.

Aidha, alisema kupitia mchezo huo yapo mapungufu kadhaa ambayo ameyaona katika safu yake ya ulinzi, hivyo atakwenda kuyafanyia kazi ili kuondoa mianya ya kupenya mipira ovyo wakati wanashambuliwa.

Naye Kocha Msaidizi wa Timu ya KMKM, Ibrahim Khamis, alisema kushindwa kufanya vizuri katika mchezo huo kulitokana na wachezaji wake kutopata muunganiko mzuri kati ya wale wapya na wazamani.

"Timu haikucheza vibaya sana, lakini tulikosa mazoezi ya pamoja kati ya wachezaji wale wapya na wazamani, na hii ni kwa sababu walichelewa kuripoti mazoezini,“ alisema huku akiahidi kuyafanyia kazi mapungufu yote ambayo ameyaona katika mchezo wao wa kwanza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### EZE ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United inamfuatilia winga wa Crystal Palace, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 26, na huenda ikamtafuta mshambuliaji huyo wa England msimu ujao. (***Manchester Evening News***)

### LIVERPOOL PIA WANAMTAKA

LIVERPOOL inaweza pia kumnunua Eberechi Eze ikiwa fowadi wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32, hatasaini mkataba mpya na klabu hiyo. (***Liverpool Echo***)

### FOFANA ATAKIWA ATHENS

CHELSEA inatarajia kumuuza mshambuliaji wa Ivory Coast, David Datro Fofana, mwenye umri wa miaka 21, kwa Klabu ya Ugiriki ya AEK Athens. Dirisha la uhamisho la Ugiriki lipo wazi hadi leo Jumatano. (***The Athletic***)

### POCHETTINO ATAJWA MAREKANI

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, anatarajiwa kuthibitishwa kuwa kocha mpya wa Marekani baada ya kukutana na wakuu wa soka wa Marekani. (***Mail***)

### ANTONY KUACHIWA UNITED

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumwachia winga wa Brazil, Antony kwa mkopo huku Fenerbahce ikiwa katika nafasi nzuri ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. (***Sun***)

### DAVIES AWANIWA GALATASARAY

KLABU ya Galatasaray ina nia ya kumsajili beki wa Tottenham Hotspur na Wales, Ben Davies mwenye umri wa miaka 31 kabla ya dirisha la uhamisho la Uturuki kufungwa Septemba 13, mwaka huu. (***Football Insider***)

### OBI ALIMSHAWISHI OSIMHEN

KIUNGO wa kati wa zamani wa Chelsea, John Obi Mikel, alijaribu kumshawishi mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, kujiunga na ,The Blues' kabla ya uhamisho wake wa mkopo kutoka Napoli kwenda Galatasaray majira ya kiangazi. (***Talksport***)

### RAMOS KUTUA CORINTHIANS

MLINZI wa zamani wa Real Madrid na Hispania, Sergio Ramos, huenda akakaribia kujiunga na Klabu ya Brazil ya Corinthians. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, amekuwa hana klabu tangu alipoondoka Sevilla majira ya joto. (***Itatiaia***)

### RABIOT KIZUNGUMKUTI

MAHITAJI ya mshahara ya kiungo Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, ni makubwa mno kwa Manchester United kumsajili Mfaransa huyo, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Juventus. (***Football Insider***)

### MELO AWEKWA SOKONI

KLABU ya Juventus bado iko tayari kupokea ofa kwa kiungo wa kati wa Brazil, Arthur Melo mwenye umri wa miaka 28, ambaye anataka kusalia na kupigania nafasi yake katika klabu hiyo. (***Fabrizio Romano***)

### DAVID AITAKA EPL

MSHAMBULIAJI wa Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24, yuko kwenye mazungumzo kuhusu mkataba mpya na Lille, lakini anaendelea kuhusishwa na kuhamia Ligi Kuu ya England, EPL. (***Teamtalk***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# 'NEYMAR NI MUHIMU BRAZIL KUTWAA KOMBE LA DUNIA'

## Rodrygo amlilia, asema yeye ni nyota wao na kitendo cha kumkosa kila mtu anaona...

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

NYOTA wa Real Madrid, Rodrygo amesema Brazil inamhitaji Neymar ikiwa wanataka kufukuzia rekodi ya kutwaa Kombe la Dunia kwa mara ya sita mwaka 2026.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye alifunga bao la kipindi cha kwanza na kusaidia Brazil kuishinda Ecuador 1-0 Ijumaa na kusimamisha msururu wao wa kupoteza mechi tatu mfululizo katika CONMEBOL za kufuzu Kombe la Dunia la 2026, alisema Neymar ni muhimu kwa mafanikio ya Brazil.

"Yeye ni nyota wetu, mchezaji wetu bora," alisema Rodrygo katika mahojiano na ESPN Brasil.

"Mtu yeyote anaweza kuiona, ni kiasi gani amekosa. Kuwa na Neymar mwenye afya, jambo ambalo sote tunataka, na yuko katika hatua za mwisho za kupona kwake. Tunataka arejeshwe haraka iwezekanavyo."

Mabingwa mara tano wa dunia, Brazil walipoteza mechi mfululizo dhidi ya Uruguay, Colombia na Argentina mwishoni mwa mwaka jana na walikuwa katika nafasi ya sita kwenye msimamo baada ya raundi sita.

Kwa ushindi huo wa Ijumaa, Brazil sasa wana pointi 10 na wako katika nafasi ya nne na jana Jumanne walitarajiwa kucheza na Paraguay mjini Asuncion.

Mfungaji bora wa muda wote wa Brazil kwa upande wa wanaume, Neymar alifanyiwa upasuaji wa kurekebisha kano za mbele katika goti lake la kushoto Novemba 2, 2023 nchini Brazil.

Amekuwa majeruhi kwa muda mrefu, ikiwa ni pamoja na majeraha kadhaa ya kifundo cha mguu wa kulia, ambayo yalimlazimu kukosa kucheza kwa wiki sita mnamo 2021 na kampeni ya ushindi ya Brazil ya Copa America 2019.

Rodrygo alisema kuwa anaendelea kuwasiliana na Neymar na kwamba anamchukulia kama mtu muhimu zaidi.

"Kila mara tunatuma ujumbe kila mmoja. Sasa anarejea kwenye mazoezi na kundi," alisema Rodrygo.

"Ni mchezaji mwenzangu, inanisikitisha sana ninapoona mtu anamsema vibaya kwa sababu ya jinsi alivyo, huwa ananitumia ujumbe, ananisaidia, nampenda."

Rodrygo alifunga mabao 10 katika mechi 34 za LaLiga msimu uliopita, na pia kuzifumania nyavu mara tano kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nafasi yake katika timu ya Real Madrid imekuwa chini ya shinikizo baada ya kuwasili kwa Kylian Mbappe, ingawa kocha Carlo Ancelotti ameendelea kumchagua kama sehemu ya safu ya ushambuliaji ya wachezaji watatu hadi sasa katika kampeni hii.

# ODEGAARD AIPA PIGO ARSENAL

**OLSO,** Norway

NAHODHA wa Norway, Martin Ødegaard, aliumia kifundo cha mguu Jumatatu kabla ya mfululizo wa michezo muhimu kwa klabu yake ya Arsenal.

Ødegaard alifunika uso wake kwa mikono alipokuwa akitibiwa uwanjani katikati ya kipindi cha pili cha ushindi wa mabao 2-1 wa Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Austria.



Alionekana ameumia vibaya kwenye kifundo cha mguu wake wa kushoto katika changamoto ngumu wakati akikabiliana na kiungo wa Austria, Christoph Baumgartner.

Ødegaard alitoka nje ya mchezo dakika mbili baadaye na kufarijiwa na mwenzake, Erling Haaland.

“Jeraha la Martin Odegaard lilionekana kuwa baya katika chumba cha kubadilishia nguo vile vile niliona alikuwa amekaa na wataalamu wa viungo karibu naye, lakini hakuwa na nafasi ya kuendelea na tunajua ilikuwa ni mshtuko wa kifundo cha mguu,“ alisema kocha wa Norway, Stale Solbakken, akimwambia mtangazaji wa TV 2.

“Ndiyo, ni kuzorota, na kama sisi tuliocheza soka tunajua, kwa bahati nzuri inaweza kuwa sawa ikiwa mishipa haijachanika.“

Daktari wa Norway, Ola Sand aliongeza kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, anaendelea vizuri, lakini MRI itatoa majibu zaidi leo.

“Martin anaendelea vizuri sasa. Amepata mkunjo mdogo wa kifundo cha mguu. Tutaona jioni nzima na kesho (leo) nini kitafuata na tutafanya nini kuhusu hilo,“ alisema Sand.

“Misukosuko ya kifundo cha mguu ni ngumu kukabiliana nayo mara moja, kwa hiyo karibu lazima tuone jinsi mambo yanavyosonga mbele.

“Tutamchunguza tukirudi hotelini. Labda tutumie ‚ultrasound‘ kuiangalia. Ikiwa hatuna uhakika, kutakuwa na MRI.“

Ødegaard alitarajiwa kurejea kutoka katika majukumu ya timu ya taifa katika wiki ngumu ya mechi za ugenini kwa Arsenal.

‚Washikabunduki‘ wanakwenda kwanza kwa wapinzani wao wa London, Tottenham Hotspur Jumapili kisha watafungua programu yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta siku nne baadaye nchini Italia.

Ziara ya Manchester City inakamilisha wiki ya kuchosha Septemba 22, mwaka huu.

## De Bruyne awabwatukia vikali wachezaji Ubelgiji

**PARIS,** Ufaransa

NAHODHA wa Ubelgiji, Kevin De Bruyne, alitoa maneno ya hasira dhidi ya wachezaji wenzake baada ya timu yake kuchapwa mabao 2-0 ugenini na Ufaransa katika mechi ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, Jumatatu.

Si kwa mara ya kwanza, De Bruyne kuonekana kuchanganyikiwa wakati wa mechi ya Kundi A2 na baadaye aliiambia televisheni ya Ubelgiji VTM kuwa mambo mengi yalikuwa yameharibika katika mchezo huo.

“Siwezi kusema hapa ni nini kilienda vibaya. Tayari nilifanya hivyo kwa timu wakati wa mapumziko,“ alisema.

“Siwezi kurudia hilo kwenye vyombo vya habari, lakini lazima liwe bora kwa kila hali. Ikiwa kiwango tunachotaka kufikia ni bora zaidi, lakini hatutoshi tena kufikia kiwango hicho, basi lazima utoe kila kitu. Usipofanya hivyo umekwisha.“

Ufaransa iliifunga Ubelgiji bao 1-0 katika mechi yao ya mwisho huku kukiwa hatarini zaidi katika hatua ya 16-bora ya michuano ya Ulaya msimu huu.

Na De Bruyne aliunga mkono maoni kama hayo Jumatatu kama alivyofanya



baada ya kuondolewa kwenye Euro nchini Ujerumani.

“Ninaweza kukubali kwamba hatuko vizuri kama mwaka 2018,“ alisema De Bruyne mwenye umri wa miaka 33, kuhusu kikosi kilichofika nusu fainali ya Kombe la Dunia nchini Urusi.

“Nilikuwa wa kwanza kuona hilo, lakini mambo mengine hayakubaliki. Sitasema nini.“

Ufaransa ilishinda mwanzo mwepesi wa kujikomboa baada ya kufungwa mabao 3-1 na Italia Ijumaa, huku bao la kufutia machozi la Randal Kolo Muani na lile la mguu wa kushoto la Ousmane Dembele kuwapa pointi zao za kwanza katika kampeni ya Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Na wakati De Bruyne alipobanwa katika mahojiano kuhusu nini kilienda vibaya, alielezea shida moja.

“Sisi ni wengi sana nyuma. Ukikaa na sita nyuma, hakuna uhusiano,“ alisema mchezaji huyo wa Manchester City.

“Ndivyo ilivyo. Si juu ya mpito, lakini kuhusu watu ambao hawatekelezi kazi zao.“

## Antony hataki kutua Fenerbahce

**MANCHESTER,** England

ANTONY amedhamiria kubaki Manchester United licha ya kutakiwa na Fenerbahce, kwa mujibu wa ESPN.

Klabu za Uturuki zinaweza kusajili wachezaji hadi Ijumaa na Fenerbahce, inayonolewa na Jose Mourinho, ni miongoni mwa wanaomwania Antony.

Winga huyo wa Brazil amecheza dakika moja pekee kati ya mechi tatu za kwanza za United za Ligi Kuu msimu huu.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba ana nia ya kucheza mara kwa mara, lakini anapendelea kubaki Old Trafford hata kama Fenerbahce watatoa ofa rasmi.

Antony, ambaye amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake, amekuwa na matatizo katika ubora wake tangu alipohama kwa pauni milioni 82 kutoka Ajax mwaka 2022.

Hata hivyo, vyanzo vimeiambia ESPN kwamba, kocha Erik ten Hag, atasita kumpoteza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, baada ya klabu hiyo kuidhinisha kuondoka kwa Jadon Sancho kwenda Chelsea siku ya mwisho ya uhamisho nchini England.

Wakati huo huo, United haitamrejesha haraka Rasmus Højlund kutoka chumba cha majeruhi, chanzo kiliiambia ESPN, hata ikiwa inamaanisha kumweka nje mshambuliaji huyo kwa muda mrefu zaidi wa wiki sita.

Højlund alipata jeraha la msuli wa paja katika mchezo wa kwanza wa ziara ya United ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani dhidi ya Arsenal Julai 28.

Klabu hiyo ilithibitisha wakati huo kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, alitarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa wiki sita.

Lakini vyanzo viliiambia ESPN kwamba United wanachukua njia ya tahadhari kwa uponaji wa Højlund, haswa kwa sababu ya wasiwasi kwamba mchezaji huyo wa Kimataifa wa Denmark hajapata faida ya kuimarisha utimamu wake wakati wa kiangazi.

Højlund aliichezea Denmark dhidi ya Ujerumani katika hatua ya 16 bora ya Euro 2024 mnamo Juni 29.

Baada ya likizo, alirejea Carrington Julai 22 na alikuwa na mazoezi ya wiki moja kabla ya kuumia katika kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Arsenal huko Los Angeles.

Amekuwa akijifua kwenye gym huko Carrington, lakini bado hajajiunga na mazoezi ya timu na kikosi cha Ten Hag.

Højlund anatazamiwa kutathminiwa tena wiki hii kabla ya safari ya kuelekea Southampton Jumamosi, lakini vyanzo vimeiambia ESPN kwamba hatashinikizwa tena kuchukua hatua hivi karibuni na mipango iko tayari kumrejesha kwa upole.

## HABARI MICHEZO

### *Mayele: Yanga hii itafika mbali CAF*

INATOKA UKURASA 24

alisema.

Mayele pia alibainisha kuwa Ligi ya Misri anakocheza ni ngumu zaidi ukilinganisha ya Tanzania.

"Ligi ya Misri ni ngumu kuliko Tanzania, ina mambo mengi sana hasa kwa wachezaji wa kigeni itakusumbua, pia kule timu karibuni zote unazocheza nazo ni ngumu sana, lakini nimeweza kupambana na nashukuru Mungu kwa sasa nimezoea," alisema straika huyo wa Pyramids, aliyemaliza nafasi ya pili kwenye ufungaji bora nchini humo akiwa na mabao 14, nyuma Wessam Abou Ali wa Al Ahly, raia wa Palestina aliyemaliza na mabao 18.



### Simba yaifuata Al Ahly Tripoli kibabe

INATOKA UKURASA 24

mbele kwenye mashindano hayo ili kutimiza malengo yao.

Wachezaji wa Simba ambao wataenda kuungana na kikosi hicho wakitokea moja kwa moja kwenye majukumu ya timu zao za taifa ni Mohamed Hussein 'Tshabalala', Ally Salim na Edwin Balua ambao wapo na kikosi cha Taifa Stars.

Mwingine ni kipa Moussa Camara ambaye yupo na kikosi cha Guinea ambacho jana kilikuwa kikicheza na Taifa Stars mchezo wa kufuzu fainali za Afrika Mataifa ya Afrika (AFCON) zitakazofanyika nchini Morocco hapo mwakani.

Mchezo huo wa Kundi H, ambao Guinea ni mwenyeji, ulichezwa jana saa 1:00 usiku nchini Ivory Coast kutokana na viwanja vya wenyeji kutokidhi vigezo vya Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Mchezo wa kwanza wa Taifa Stars uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa wiki iliyopita dhidi ya Ethiopia, Stars ililazimishwa suluhu baada ya kumaliza dakika 90 bila kufungana dhidi ya Ethiopia.

# GIDABUDAY KUZIKWA KATESH JUMAMOSI, BMT, RT WAMLILIA

**Na Waandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa zamani wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Wilhelm Gidabuday, aliyefariki dunia usiku wa kuamkia jana kwa ajali ya gari jijini Arusha, anatarajiwa kuzikwa Jumamosi kijijini kwao, Nangwa wilayani Katesh, Manyara.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na shirikisho hilo, ilieleza kuwa kwa sasa msiba wa kiongozi huyo wa zamani wa RT, upo nyumbani wake, Maroroni, Maji ya Chai mkoani Arusha.

"Msiba wa kiongozi wa zamani wa RT upo nyumbani kwake Maroroni, Maji ya Chai, Arusha na mazishi yake yanatarajiwa kufanyika Jumamosi Septemba 14, kijijini kwao, Nangwa, Katesh mkoani Manyara," ilieleza taarifa hiyo iliyotolewa na Idara ya Habari ya Shirikisho ya RT.



Gidabuday

Wakati huo huo, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), limeeleza kusikitishwa na kifo hicho, likisema taifa limepoteza mtu muhimu kwenye nyanja ya riadha.

Katika salamu zake kwenda kwa RT, BMT imetoa pole kwa shirikisho hilo kwa familia na wadau wa riadha nchini.

"Baraza la Michezo (BMT), linatoa pole kwa familia na wadau wa riadha nchini kufuatia kifo cha aliyewahi kuwa Katibu wa Shirikisho la Riadha Tanzania, Gidabuday kilichotokea Septemba 10, mkoani Arusha, Bwana Ametoa, Bwana Ametwaa, jina lake lihimidiwe," ilisema BMT katika salamu zake za rambirambi.

Kwa mujibu wa Mjumbe wa Riadha Kanda ya Mashariki, Alfredo Shahanga, kiongozi huyo wa zamani wa shirikisho hilo alifariki dunia saa 7:00 usiku wa kuamkia jana kwa kugongwa na gari jijini Arusha, eneo la Majani ya Chai.

"Ni kweli Gidabuday hatunaye, alipata ajali ya gari, na kwa mujibu wa mashuhuda ni kwamba alifariki dunia hapo hapo, ni masikitiko makubwa kwetu na wapenda michezo, si wa riadha tu, bali michezo yote," alisema Shahanga kwa masikitiko.

Gidabuday, aliutwaa Ukatibu Mkuu wa RT mwaka 2016 katika uchaguzi Mkuu kwa kupata kura 38 na kumshinda mpinzani wake mkubwa, Michael Washa, aliyepata kura 24, na alidumu kwenye kiti hicho hadi 2019, alipojiuzulu mwenyewe kwa kile alichokisema kuwa ni kwa manufaa ya mchezo huo.

Alijiuzulu bila shinikizo lolote na kumkabidhi madaraka Ombeni Zavalla, akiwataka viongozi wengine waige mfano wake.

Akiwa madarakani alifanikiwa kutwaa medali mbili za Shaba zilizoletwa na mwanariadha Alphonce Simbu katika mashindano ya Dunia ya 2017 nchini Uingereza, na Francis Damiano, aliyeshinda medali kama hiyo kwenye Michezo ya Jumuiya ya Madola kwa Vijana mwaka huo huo nchini Bahamas.

Kabla na baada ya madaraka, Gidabuday, alikuwa akiuishi mchezo huo, mara kwa mara akitoa mawazo yake kwenye vyombo vya habari kuhusu maendeleo ya mchezo wenyewe na hata kukosoa baadhi ya mienendo ya viongozi kama akiona mambo hayaendi sawa.

# Kagera Sugar kuanza kukusanya pointi

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kuanza vibaya Ligi Kuu kwa kupoteza michezo yote miwili ya mwanzo, kikosi cha Kagera Sugar leo kina kibarua kingine cha kusaka alama tatu dhidi ya Tabora United.

Kagera itakuwa ugenini kwenye mchezo huo na kocha wa timu hiyo, Paul Nkata, amesema wanataka kuanza kukusanya pointi kuanzia kwenye mchezo huo.

"Hatuna rekodi nzuri kwenye michezo yetu miwili iliyopita, lakini tumeendelea kujiimarisha na kufanyia kazi mapungufu yetu, naamini kuanzia mchezo wa kesho (leo), tutaanza kupata matokeo mazuri," alisema Nkata.

Alisema moja ya sababu iliyowafanya kushindwa kuvuna pointi kwenye michezo yao miwili iliyopita, ni umakini mdogo kwenye kuzitumia nafasi wanazozitengeneza.

"Tumekuwa tukicheza vizuri na kujitahidi kutengeneza nafasi za kutosha, lakini tumekuwa na umaliziaji mbovu, hili nililiona na tumekuwa tukilifanyia kazi kwenye uwanja wa mazoezi," alisema Nkata.

Aidha, alisema katika mazoezi ya hivi karibuni, safu yake ya ushambuliaji imeendelea kuimarika na kuonesha matumaini ya kupata mabao kwenye michezo inayofuata.

Kikosi hicho cha Kagera juzi kilicheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Geita Gold na kuambulia sare ya bao 1-1.

Katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu inayorejea tena leo, Fountain Gate itaumana na Kengold FC na kufanya leo kuwa na michezo miwili ya ligi hiyo.

Michezo

Nipashe

Jumatano Septemba 11, 2024



## Gidabuday kuzikwa Katesh Jumamosi

UKURASA 23

### UNAPENYA JE!...



Mlinda usalama uwanjani ('Steward'), akiruka kumzuia shabiki aliyevamia uwanjani (pitch invader) kwenda kumkumbatia, mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, kwenye mechi ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya dhidi ya Scotland, iliyopigwa Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Estadio da Luiz uliopo Benfica, Ureno. Wenyeji hao walishinda kwa mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# MAYELE: YANGA HII ITAFIKA MBALI CAF

## ●●● Akunwa na usajili wa malengo uliofanywa huku akivutiwa pia na viwango vya...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA za zamani wa Yanga, Fiston Mayele, amekisifu kikosi cha timu hiyo msimu huu, akisema ni kizuri, chenye wachezaji bora wenye njaa ya mafanikio, akikitabiria kufika mbali kwenye michuano ya kimataifa.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Mayele alisema usajili uliofanyika msimu huu, licha ya kwanza haukuwa mkubwa sana, lakini umeongeza wachezaji bora ambao wameenda kuungana na wengine wenye kiwango cha juu na kuifanya kuwa tishio si Tanzania tu bali Afrika.**

Mayele alisema hayo baada ya kumaliza mchezo kati ya Timu yake ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Ethiopia wa kuwania tiketi ya kucheza fainali za Mataifa Afrika (AFCON), mwakani nchini Morocco, uliochezwa juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, akifunga bao la pili dakika ya 76, baada ya Theo Bongonda kupachika la kwanza dakika ya 62.

Ethiopia, ambayo walitoka suluhu dhidi ya Tanzania, Jumatano iliyopita kwenye uwanja huo, waliutumia tena safari hii kama wao wa nyumbani kutokana na viwanja nchini mwao kutokidhi viwango vya Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

"Yanga imefanya usajili mzuri sana, ina wachezaji wazuri, wanacheza kwa kasi na morali kubwa, msimu uliopita walisajili vizuri na msimu huu pia wamesajiliwa wachezaji wazuri, na hili nimeshawahi kumwambia Rais wa Yanga, Injinia Hersi, nilimpongeza kwa usajili bora na yeye pia alinipongeza kwa kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu nchini Misri.

"Msimu huu wameongeza wachezaji wachache ambao nawatakia kila laheri kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu, kama wataendelea kupambana hivi watafanya vema na kufika mbali," alisema Mayele.

Straika huyo aliyeichezea Yanga kuanzia 2021 hadi 2023 kabla ya kuhamia Pyramids ya Misri, amebainisha kuwa inawezekana kuna siku anaweza kurejea Tanzania kwa sababu kwake anaona ni kama nyumbani.

"Nimefurahi sana kurudi hapa, Tanzania ni nyumbani, na hata kufahamika zaidi nimefahamika kutokea hapa, Mungu akipenda ipo siku naweza kurejea,"

INAENDELEA UK. 23

## Simba yaifuata Al Ahly Tripoli kibabe

**Faustine Feliciane na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha wachezaji 18 wa Simba kimeondoka nchini alfajiri ya leo kuelekea Libya tayari kwa mchezo wa kwanza wa raundi ya kwanza wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema wachezaji 18 wataondokea hapa nchini na wengine wanne ambao wapo kwenye majukumu ya Timu za Taifa za Tanzania na Guinea, wataungana na wenzao Libya moja kwa moja kesho wakitokea kwenye timu zao.

"Kikosi kipo tayari, kinaondoka kesho (leo) alfajiri, Libya tutakuwa na wachezaji 22, wengine wanne watakuja kuungana na sisi moja kwa moja Libya baada ya kumaliza majukumu yao kwenye timu zao za taifa," alisema Ahmed.

Aidha, alisema kocha wa timu hiyo, Fadlu Davids, amesema kikosi kimekamilika na wamejiandaa vizuri kupata ushindi kwenye mchezo huo wa ugenini.

"Kwenye mazoezi ya mwisho kocha ameridhishwa na maandalizi, wachezaji wake wapo kwenye morali kubwa kuelekea kwenye mchezo huo, kwa kifupi Wanasimba tuna matumaini makubwa na kikosi chetu kuelekea kwenye mchezo huo.

"Wachezaji wetu wapo vizuri kuelekea kwenye mchezo huo ambao tunaamini utakuwa na upinzani mkubwa, lakini kwa upande wetu tupo vizuri idara zote," aliongeza Ahmed huku akibainisha kuwa malengo yao ni kwenda kufanya vizuri na kuweza kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kupitia mchezo wao huo.

Alisema Fadlu amekuwa wakiwapa wachezaji mazoezi ya nguvu ambayo anaamini yameimarisha miili ya wachezaji kuelekea mchezo huo.

Alisema morali ya kila mchezaji ipo juu katika kuhakikisha wanafanya vizuri na kusonga

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042